VOL. LIII, No. 41

13 OKTOBA, 1972

MAONI YA MPIGACHAPA
—O—
SOMA GAZETI
LA
SERIKALI SASA

JAMHURI YA MUUNGANO
WA TANZANIA

—O—

GAZETI

DAR ES SALAAM

KWA KUIKUZA
LUGHA YAKO
YA TAIFA
—O—
(KISWAHILI)

BEI SH. 1/25

Linatolewa kwa Idhini ya Serikali na limeandikishwa Posta kama Gazeti

YALIYOMO

	Taarifa ya Kawaida	Uk.
Kuajiriwa na Kukabidhiwa Madaraka, n.k. ...	Na. 1454	623
Notice *re* Supplement	Na. 1455	624
Tanzia		624
Katika Mahakama ya Rufani ya Afrika Mashariki—Orodha ya Rufani	Na. 1456	624
Uteuzi wa Wajumbe wa Mipango	Na. 1457	624
Tangazo—Tanzania Stocks	Na. 1458	624
Tangazo—Idara ya Reli ya Afrika Mashariki ...	Na. 1459	624
Matokeo ya Uchaguzi wa Madiwani, 1972	Na. 1460	624
Maombi ya Mitihani ya Mwaka 1973	Na. 1461	625
Wakuu wa Dini Walioruhusiwa Kufungisha Ndoa	Na. 1462	625
Ofisi ya Bodi Kuu ya Tenda—Matangazo ya Tenda	Na. 1463–4	625
Bodi ya Tenda ya Mkoa wa Arusha—Tenda za Utoaji wa Kokoto	Na. 1465	625
Bahati Nasibu ya Taifa—Tangazo la Ushindi wa Mchezo wa 8/72	Na. 1466	625
Akiba ya Watumishi wa Tawala za Mitaa ...	Na. 1467–8	626/7
Benki Kuu ya Tanzania—Mizania kama Ilivyokuwa Tarehe 31 Julai, 1972	Na. 1469	628
Wahakiki wa Madini Walioandikishwa	Na. 1470	628
Vyama Vilivyoandikishwa	Na. 1471	628
Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi—Mikataba ya Hiari	Na. 1472–4	629/31
Ubatilisho wa Haki ya Kumiliki Ardhi	Na. 1475	632
Kupotea kwa Kitabu cha Kuagizia Vifaa	Na. 1476	632
Kupotea kwa Hati za Bima	Na. 1477–8	632
Maombi ya Leseni za Magari ya Abiria, n.k. ...	Na. 1479	633
Baraza la Leseni za Usafirishaji—Kusikiliza Maombi	Na. 1480	634
Makampuni Yanayotarajiwa Kufutwa katika Daftari la Makampuni	Na. 1481	635
Mtumizi wa Alama ya Biashara	Na. 1482	635
Tangazo la Kuuza Biashara	Na. 1483	635
Taarifa	Na. 1484	635

KUAJIRIWA NA KUKABIDHIWA MADARAKA

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 1454

Ofisi ya Rais:

Kuwa Mkuu wa Chuo, Ujuzi:—

A. MURASI, Kaimu Mkuu wa Chuo, kuanzia tarehe 1 Agosti, 1972.

Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais:

Kuwa "Statistical Clerk":—

D. L. M. M. MOLLEL, kuanzia tarehe 13 Julai, 1972.

Kuwa "Executive Officers":—

R. L. M. SAFARI, kuanzia tarehe 6 Agosti, 1972.
R. A. MUNUO, kuanzia tarehe 26 Juni, 1972.
S. J. H. SABUNI, kuanzia tarehe 19 Juni, 1972.
T. M. E. K. KAKOME, kuanzia tarehe 17 Julai, 1972.

Wizara ya Mali ya Asili na Utalii:

Kuwa Bwana Misitu Msaidizi, daraja la II:—

K. M. E. URIO, kuanzia tarehe 4 Julai, 1972.

Kuwa Bwana Miti Msaidizi, daraja la II:—

S. B. C. MREMA, kuanzia tarehe 1 Julai, 1972.

Kuwa Afisa Msaidizi wa Nje (Nyuki), daraja la II:—

N. KAWA, kuanzia tarehe 1 Julai, 1972.

Wizara ya Biashara na Viwanda:

Kuwa "Laboratory Assistant":—

M. L. L. GANYARA, kuanzia tarehe 6 Juni, 1971.

Kuwa Bwana Shamba Msaidizi wa Migodi:—

W. N. LYOMBE, kuanzia tarehe 10 Juni, 1971.

Kuwa Makarani:—

H. A. RUSHAKA, kuanzia tarehe 24 Agosti, 1972.
S. O. MSOWOYA, kuanzia tarehe 31 Agosti, 1972.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi:

Kuwa Mratibu Mkuu wa Polisi:—

D. ABDALLAH, kuanzia tarehe 1 Mei, 1972.

Kuwa Makarani:—

E. G. KABEREGE, kuanzia tarehe 18 Mei, 1972.
M. P. G. KABATA, kuanzia tarehe 12 Septemba, 1972.
M. T. MULLO, kuanzia tarehe 15 Septemba, 1972.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo Mijini:

Kuwa Karani:—

F. A. NYONI, kuanzia tarehe 1 Aprili, 1972.

Mahakama Kuu:

Kuwa Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo, daraja la I:—

A. M. HAMISI, Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo, daraja la II, kuanzia tarehe 1 Mei, 1972.

Matangazo yahusuyo mali za watu waliofariki, kuvunja mikataba ya ushirikiano na mengineyo, yakiwa ya manufaa kwa umma, yaweza kuchapishwa katika *Gazeti*. Matangazo yote yapelekwe kwa **Mhariri, Idara Kuu ya Utumishi wa Serikali, Ofisi ya Rais, S.L.P. 2483, Dar es Salaam,** *kabla ya Jumatatu ya kila juma*. **Matangazo yasitumwe kwa Mpigachapa Mkuu wa Serikali.**

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 1455

Notice is hereby given that Orders, as set out below, have been issued and are published in Subsidiary Legislation Supplement No. 59 to this number of the *Gazette*:—

Kanuni ya Kima cha Mishahara na Masharti ya Kazi ya 1972 (Government Notice No. 208 of 1972).

Order under the Rule Against Perpetuities (Limitation of Application) Act, 1969 (Government Notice No. 209 of 1972).

Order under the Rule Against Perpetuities (Limitation of Application) Act, 1969 (Government Notice No. 210 of 1972).

Order under the Companies Ordinance (Government Notice No. 211 of 1972).

TANZIA

Mtukufu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo kilichotokea kwa ajali ya gari barabarani, Manzese, Dar es Salaam, tarehe 25 Julai, 1972 cha Bw. A. S. KIROBOTO, Fundi Chapa Mwanafunzi, Idara ya Kupiga Chapa, Wizara ya Habari na Utangazaji.

Mtukufu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo kilichotokea katika Hospitali ya Mbeya, tarehe 22 Septemba, 1972 cha V. C. O. SIKIRA, Mkaguzi wa Kodi, Wizara ya Fedha.

Mtukufu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha Bwana S. M. MAHIMBWA, aliyekuwa Katibu Tarafa wa Mkongo, katika Wilaya ya Rufiji, kilichotokea tarehe 1 Oktoba, 1972. Mazishi yakafanyika tarehe 2 Oktoba, 1972.

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 1456 JY/C. 210/1/685

KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI YA AFRIKA YA MASHARIKI, DAR ES SALAAM

ORODHA YA RUFANI

Jumanne tarehe 17 Oktoba, 1972 saa tatu kamili

Mbele ya Waheshimiwa SPRY, *Kaimu Rais;* LAW, *Kaimu Makamu wa Rais na* LUTTA, *Jaji wa Rufani*

Kwa kusikilza:	*Rufani za Jinai:*
Na. 14/72 (W)	Jamhuri na Iddi Hamisi Migila.
Na. 84/72 (W)	Jamhuri na Sebastiano Mkwe.
Na. 48/72	Jamhuri na Rogasian Salasini.

Jumatano tarehe 18 Oktoba, 1972 saa tatu kamili

Na. 85/72 (W)	Jamhuri na Clemence N. Mziray.
Na. 92/72 (W)	Jamhuri na Ali Mohamed Pirbhai Kassam.
Na. 102/72	Jamhuri na Emmanuel Barongo.
Na. 109/72	Jamhuri na Kolincli Mwakabuli.

Alhamisi tarehe 19 Oktoba, 1972 saa tatu kamili

Na. 90/72 (W)	Jamhuri na Makonomalonja Nyanda.
Na. 110/72 (W)	Jamhuri na Solomon Ulaya.
Na. 63/72	Jamhuri na Absolom Homel Mwakyusa.
Na. 76/72	Jamhuri na Mlefu Kuleja.

Ijumaa tarehe 20 Oktoba, 1972 saa tatu kamili

Na. 91/72 (W)	Jamhuri na Kabinga Iringa.
Na. 97/72	Jamhuri na Frank D. Kachile.
Na. 98/72	Jamhuri na Saidi Polindani.
Na. 115/72	Jamhuri na Saidi Omari.

Jumatatu tarehe 23 Oktoba, 1972 saa tatu asubuhi

Kwa kusikiliza:	*Rufani ya Madaawa:*
Na. 19/72	Zambia-Tanzania Road Services Ltd. na mwingine na Nduku Mutua.
Na. 53/72	Habib M. Yusufali na Abdulsattar Riazid-din.

Jumanne tarehe 24 Oktoba, 1972 saa tatu asubuhi

Na. 50/72	Hatimali Adamji na East African Posts and Telecommunications Corporation.

Nairobi,
2 Oktoba, 1972

T. T. M. ASWANI,
Mrajis

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 1457

UTEUZI WA WAJUMBE WA TUME YA MIPANGO

The Planning Commission Act, 1972

(No. 28 of 1972)

1. Inatangazwa kwa watu wote kwamba kwa kufuata masharti ya fungu la 4 la Sheria ya Tume ya Mipango ya 1972, Mtukufu Rais amewateua watu hawa wafuatao wawe Wajumbbe wa Tume ya Mipango:—

Mwenyekiti: Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais.

Makamu wa Mwenyekiti: Waziri wa Mambo ya Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Wajumbe wa Tume: Watu wote ambao kwa wakati huu ni Wabunge.

Katibu wa Tume: Katibu Mkuu, Wizara ya Mambo ya Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

2. Mtukufu Rais ameichagua Wizara ya Mambo ya Uchumi na Mipango ya Maendeleo iwe ndiyo Wizara itakayotoa huduma-za kiofisi kwa Tume ya Mipango.

Katibu,
Dar es Salaam *Tume ya Mipango*

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 1458

TANGAZO

6 PER CENT TANZANIA STOCK, 1972

6½ PER CENT TANZANIA STOCK, 1974/76

6¾ PER CENT TANZANIA STOCK, 1980/81

6½ PER CENT TANZANIA STOCK, 1987

Malipo ya faida kwa dhamana zilizotajwa hapo juu yatafanywa tarehe 14 Novemba, 1972. Kwa ajili ya utayarishaji wa hundi za malipo ya faida, vitabu vya uandikishaji we dhamana hizo vitafungwa tarehe 14 Oktoba, 1972 jioni na baada ya siku hiyo dhamana zitauzwa ama kununuliwa bila malipo ya faida.

Benki Kuu ya Tanzania,
S.L.P. 2939,
Dar es Salaam,
7 Oktoba, 1972

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 1459

TANGAZO

IDARA YA RELI YA AFRIKA MASHARIKI

KITABU CHA UCHUKUZI NAMBARI 5

Karati ya masahihisho Nambari 24 ya Kitabu cha Uchukuzi Nambari 5 imepigwa chapa na imepelekwa kwa wote ambao wamo katika orodha yetu ya wale wenye Kitabu hiki. Mabadiliko yote yaliyofanywa kuhusu Kitabu cha Uchukuzi tokea kutolewa kwa karatasi ya masahihisho Nambari 23 yamo katika karatasi hiyo mpya (yaani Nambari 24).

Ye yote mwenye Kitabu cha Uchukuzi Nambari 5 ambaye hajapata bado karatasi hii ya mabadilisho mpaka hapo tarehe mosi mwezi wa Oktoba, anaombwa amuarifu Mkuu wa Usafirishaji (yaani Chief Traffic Manager), Shirika la Reli ya Afrika Mashariki, Sanduku la Posta 30006, Nairobi. Karatasi hiyo ya mabadilisho yaweza pia kuonekana katika ofisi zetu za kununua tikiti kuanzia tarehe mosi mwezi wa Oktoba, 1972.

The Chief Traffic Manager,
E.A. Railways and Harbours,
P. O. Box 30006,
Nairobi

S. NGUNU,
k.n.y. Mkurugenzi wa Idara ya Reli

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 1460 TU/R/10/11/56

MATOKEO YA UCHAGUZI WA MADIWANI, 1972

Sheria ya Uchaguzi

(Kifungu cha 96 (d))

Inatangazwa kwa ufahamisho wa watu wote kwamba kwa mujibu wa kifungu cha 96 cha Sheria ya Uchaguzi, matokeo ya uchaguzi wa Madiwani uliofanyika kwa kufuata Taarifa ya Kawaida Na. 1095 ya tarehe 4 Agosti katika Wadi zilizofanya uchaguzi ni kama ifuatavyo:—

HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA

Majina ya Wagombea Uchaguzi	*Idadi ya Kura*
Namba IV:	
Wadi: Kalebezo.	
Andrew Robert Nkanga	144
Nghalingi Timetheo Mabelemanonu	81
Aliyechaguliwa: A. R. Nkanga.	
Namba XXXIV:	
Wadi: Ikina.	
Abdallah Mate Buhabi	200
Zacharia Masesa Mzelela	72
Aliyechaguliwa: Bwana A. M. Buhabi.	

HALMASHAURI YA WILAYA YA MANYOVU

Namba XI:	
Wadi: Ikasi.	
Cosmas Chitulo Chisande	46
Nyamiyahe Samueli Mbuni	216
Aliyechaguliwa: Bwana N. S. Mbuni.	
Namba XXV:	
Wadi: Kitembe.	
Manyale Daniel Paulo	443
Ombogo Onyona Harison	676
Aliyechaguliwa:: Bwana O. O. Harison.	

HALMASHAURI YA WILAYA YA MTWARA

Namba XV:	
Wadi: Nambu.	
Mussa Mohamed Kaisi	292
Sangulisa Hamisi Selemani	243
Aliyechaguliwa: Bwana M. M. Kaisi.	

HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE

Namba XV:

Wadi: Chitele.

Cramwell Mtafka	185
Mwakapenda Enosi	200

Aliyechaguliwa: Bwana M. Enosi.

Dar es Salaam,
29 Septemba, 1972

B. R. KIMALANDO,
Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 1461 C. 43/SF. 1/779

MAOMBI YA MITIHANI YA MWAKA 1973

CHETI CHA UPIMAJI WA ARDHI CHA AFRIKA MASHARIKI

Maombi yanakaribishwa kwa ajili ya mitihani ya KATI na ya MWISHO ambayo itafanyika mnamo mwezi wa Februari, 1973. Waombaji wote watahitajiwa kujaza fomu ambazo zinapatikana kutoka kwa wafuatao:—

Kenya:

The Director of Surveys,
Survey of Kenya,
P.O. Box 30046,
Nairobi, Kenya.

Uganda:

The Commissioner for Lands & Surveys,
P.O. Box 7061,
Kampala, Uganda.

Tanzania:

The Commissioner for Surveys & Mapping,
P.O. Box 9201,
Dar es Salaam.

Fomu zote ni lazima zirudishiwe waliotajwa kabla ya tarehe 30 Novemba, 1972.

Idara ya Upimaji na Ramani,
S.L.P. 9201,
Dar es Salaam,
5 Oktoba, 1972

E. N. NJAU,
Katibu,
Bodi ya Kusimamia Mitihani ya Upimaji wa Ardhi, Afrika Mashariki

---

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 1462

WAKUU WA DINI ZILIZOTAJWA AMBAO WAMERUHUSIWA KUFUNGISHA NDOA

Sheria ya Ndoa 1971

Katika kutumia mamlaka niliyopewa na fungu la 30 la Sheria iliyotajwa hapo juu, Wakuu wa Dini wanaotajwa hapa chini wanaruhusiwa kufungisha ndoa katika Tanganyika:—

Na. C.419.
Jina: Father LUDOVICUS MDENKERI.
Madhehebu ya Dini: Roman Catholic.

Na. C.420.
Jina: Reverend Father MUHIGWA PETER.
Madhehebu ya Dini: Roman Catholic.

Na. C.421.
Jina: PASTOR ZIMBEIYA.
Madhehebu ya Dini: Roman Catholic.

Na. C.422.
Jina: LUCAS MICHAEL KYESSI.
Madhehebu ya Dini: Lutheran.

Na. C.423.
Jina: ASUKILE S. MWAIKENDA.
Madhehebu ya Dini: Pentecostal Holiness Association Mission.

Na. C.424.
Jina: LAWRENCE M. MWAKATAGE.
Madhehebu ya Dini: Pentecostal Holiness Association Mission.

Na. C.425.
Jina: FILIPO NGHOLOPE.
Madhehebu ya Dini: Swedish Free Mission.

Na. C.426.
Jina: DOMENICO ALTIERI.
Madhehebu ya Dini: Roman Catholic.

Dar es Salaam,
5 Oktoba, 1972

V. O. SLESSER,
Msajili Mkuu wa Ndoa

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 1463

OFISI YA BODI KUU YA TENDA

TENDA NA. 51 YA 1972/73

TENDA YA NETS MOSQUITO

1. Maombi ya tenda yanakaribishwa kwa kuiuzia Serikali vifaa vilivyotajwa hapa chini na kupelekwa Bohari Kuu ya Serikali, S.L.P. 9150, Dar es Salaam.

Maelezo	*Idadi*
(a) Nets mosquito household white size: 82" x 48" x 84"	40,000
(b) Nets mosquito bed camp green of size: 7' 0" x 3' 0" x 4' 6"	10,000
(c) Nets mosquito sand fly jungle green of size: 6' 6" x 3' 0" x 4' 3"	10,000

2. Maelezo zaidi ya tenda hii yanapatikana kwa Mwandishi, Bodi Kuu ya Tenda, S.L.P. 49, Dar es Salaam.

3. Tarehe na muda wa kufungwa kwa tenda hii ni saa tatu (3) asubuhi, siku ya Ijumaa, tarehe 17 Novemba, 1972.

Dar es Salaam,
29 Septemba, 1972

Mwandishi,
Bodi Kuu ya Tenda

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 1464

OFISI YA BODI KUU YA TENDA

TENDA NA. 34 YA 1972/73

TENDA YA KUNYUNYIZA DAWA KWA NDEGE

1. Maombi ya tenda yanakaribishwa na Wizara ya Kilimo kwa kazi ya kunyunyiza dawa kwa ndege (Aerial Spraying of Quelea Birds—Sudan Dioch).

2. Maelezo zaidi ya tenda hii yanapatikana kwa Mwandishi, Bodi Kuu ya tenda, S.L.P. 49, Dar es Salaam.

3. Muda na tarehe ya kufungwa kwa tenda hii ni saa 3 (tatu) asubuhi, siku ya Ijumaa, tarehe 10 Novemba, 1972.

Dar es Salaam,
30 Septemba, 1972

Mwandishi,
Bodi Kuu ya Tenda

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 1465 ARU/6/3/1972/73/47

BODI YA TENDA YA MKOA WA ARUSHA

TENDA ZA UTOAJI WA KOKOTO

1. Tenda zinakaribishwa kwa utoaji wa kokoto kwenye barabara za Mkoa wa Arusha.

2. Bei ni lazima ziwe pamoja na utoaji wa kokoto, kupakia na kupeleka mahali panapotakiwa.

3. Bei tofauti ni lazima zionyeshwe kwa kokoto za ½" na ¾" kama ifuatavyo hapa chini.

Location:

(a) Mile 21 mpaka 22½—1½ mile.
Njia ya Arusha-Babati. Jumla mizigo 60 ya 5 cubic yard kila moja kokoto za ½" au ¾".

(b) Mile 23 mpaka 26—2½ mile.
Njia ya Arusha-Babati. Jumla mizigo 100 ya 5 cubic yard kila moja kokoto za ½" au ¾".

(c) Mile 52 mpaka 56—4 mile.
Njia ya Arusha-Babati. Jumla mizigo 160 ya 5 cubic yard kila moja kokoto za ½" au ¾".

(d) Mile 61 mpaka 62½—1½ mile.
Njia ya Arusha-Babati. Jumla mizigo 60 ya 5 cubic yard kila moja kokoto za ½" au ¾".

(e) Mile 22 mpaka 24 mile.
Njia ya Arusha-Moshi. Jumla ya mizigo 80 ya 5 cubic yard kila moja kokoto za ½" au ¾".

4. *Specifications:*

All chippings supplied should confirm to the following:—

(a) ½ will pass through ½" sieve and retained in ⅜" sieve.
(b) ¾ will pass through ¾" sieve and retained in ½" sieve.
(c) All agregate must be crushed from good hard stones and free from dust, organic matter or other impurities.
(d) Sample of chippings must accompany each tender, and in the event of contract being late, delivery must not fall below the standard of the sample.

5. Maombi yakiwa katika bahasha iliyofungwa (Sealed) na kuandikwa juu yake "Tenda ya Utoaji Kokoto" yatumwe kwa Mwandishi, Bodi ya Tenda Mkoani Arusha, S.L.P. 601, Arusha.

6. Mwisho wa kupokea tenda hii ni tarehe 24 Oktoba, 1972, saa tano kamili.

Arusha,
29 Septemba, 1972

Mwandishi,
Bodi ya Tenda Mkoani

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 1466 TSL/D. 20/8/72/15

BAHATI NASIBU YA TAIFA—TANZANIA

TANGAZO LA USHINDI WA MCHEZO WA 8/72 ULIOCHEZWA TAREHE 3 OKTOBA, 1972, DAR ES SALAAM

Zawadi ya Kwanza Sh. 25,000/- Tikiti Na.	094975
Zawadi ya Pili Sh. 15,000/- Tikiti Na.	091297
Zawadi ya Tatu Sh. 8,000/- Tikiti Na.	055622
Zawadi 15 kila moja Sh. 2,000/-:—	
1. Tikiti Na.	012548
2. Tikiti Na.	015377
3. Tikiti Na.	017932
4. Tikiti Na.	022547
5. Tikiti Na.	025484
6. Tikiti Na.	031633
7. Tikiti Na.	032204
8. Tikiti Na.	044813
9. Tikiti Na.	081215
10. Tikiti Na.	093948
11. Tikiti Na.	121988
12. Tikiti Na.	132356
13. Tikiti Na.	137256
14. Tikiti Na.	144023
15. Tikiti Na.	148342
Zawadi 150 za Sh. 100/- kila moja kwa tikiti zote zinazoishia nambari	438
Zawadi 1,500 za Sh. 10/- kila moja kwa tikiti zote zinazoishia nambari	20
Zawadi 15,000 za Sh. 6/- kila moja kwa tikiti zote zinazoishia nambari	2

Mwisho wa malipo kwa tikiti zinazoshinda katika mchezo huu ni tarehe 1 Aprili, 1973.

Zawadi za Sh. 100/- na kwenda chini zitalipwa na Ofisi ya Fedha yo yote ya Serikali, Tanzania.

Wizara ya Fedha,
S.L.P. 9111,
Dar es Salaam,
4 Oktoba, 1972

M. S. KHARUSI,
Mkurugenzi Msaidizi wa Bahati Nasibu ya Taifa

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 1467

AKIBA YA WATUMISHI WA TAWALA ZA MITAA

HESABU ZA AMANA NA MALIPO KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 30 JUNI, 1969

1967/68 Sh.	St.	AMANA	1968/69 Sh.	St.	1967/68 Sh.	St.	MALIPO	1968/69 Sh.	St.
41,377,837	25	Baki ya kuioka nyuma ...	50,332,571	90	4,524,632	20	Malipo	4,320.988	30
5,823,972	50	Amana zilizopokelewa ...	6,061,416	25	50,332,571	90	Baki	60,420,079	55
5,823,972	50	Kisutuo	6,061,416	25					
1,831,421	85	Ziada iliyolipwa kwa walimbikaji	2,285,663	45					
54,857,204	10		64,741,067	85	54,857,204	10		64,741,067	85

MALIPO NA MATUMIZI KWA MWAKA ULIOSHIA TAREHE 30 JUNI, 1969

MATUMIZI					MAPATO				
75,421	75	Matumizi ya usimamizi ...	67,212	50	2,898,126	10	Faida iliyotokana na Dhamana za Serikali ya Tanzania	3,360,258	20
1,831,421	85	Ziada liyolipwa kwa Walimbikaji	2,285,663	45	2,148	60	Faida iliyotokana na kuigomboa Dhamana ya Serikali ya Tanzania 6½ kwa mia 1967/68	—	—
14,756	80	Gharama za Benki	14,284	35	45,500	00	Faida ambayo haijapokelewa Dhamana ya Serikali ya Tanzania 6½ kwa mia 1975/78	45,500	00
1,024,174	30	Mapato yaliyozidi matumizi ...	1,038,597	90					
2,945,774	70		3,405,758	20	2,945,774	70		3,405,758	20

MIZANIA KAMA ILIVYOKUWA TAREHE 30 JUNI, 1969

DHIMA					MALI				
50,332,571	90	Baki ya Walimbikaji	60,420,079	55	70,597	10	Fedha iliyoko Benki	1,817,635	65
1,957,978	10	Mlimbiko wa faida	1,957,978	10			Dhamana za Serikali ya Tanzania		
		Jumlisha na mapato yaliyozidi	2,996,576	00	47,268,745	30	inayojulikana bei tarehe 30.6.69....	54,604,354	90
		matumizi	1,038,597	90			Sh. 57,748,268.00		
					2,448,300	00	Dhamana nyinginezo za Serikali ya Tanzania	2,448,300	00
					2,457,407	60	Amana na Visutuo ambavyo havijalipwa	4,500,865	00
					45,500	00	Faida ambayo haijapokelewa Dhamana ya Serikali ya Tanzania 6½ kwa mia 1975/78	45,500	00
52,290,550	00		63,416,655	55	52,290,550	00		63,416,655	55

Hesabu za mapato na matumizi pamoja na mizania zilizo hapo juu zimakaguliwa kulingana na yaliyomo katika kifungu cha 3(6) cha Sheria ya Akiba ya Watumishi wa Tawala za Mitaa. Nimepata habari pamoja na maelezo yote niliyohitaji. Kwa hiyo ninathibitisha baada ya Ukaguzi huu kwamba, kwa maoni yangu hesabu hizo ni sawa; isipokuwa njia iliyotumiwa kwa kutoa faida inahitilafiana na ile iliyo katika sheria iliyotajwa hapo juu.

Urban Council Division,
Magogoni Road,
P.O. Box 2400,
Dar es Salaam,
6 Septamba, 1972

S. M. MABEYO,
Katibu,
Halmashauri Kuu,
Akiba ya Watumishi wa Tawala za Mitaa

E. A. MULOKOZI,
Mwenyekiti,
Halmashauri Kuu,
Akiba ya Watumishi wa Tawala za Mitaa

A. S. KAPANGE,
Kaimu wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu

LOCAL AUTHORITIES PROVIDENT FUND INVESTMENTS AS AT 30TH JUNE, 1969

Stock	Value Nominal (Face Value)	Book (Cost Value)	Middle Market Price	Value as at 30th June, 1969	Appreciation	Depreciation
	Shs. Cts.	Shs. Cts.		Shs. Cts.	Shs. Cts.	Shs. Cts.
1. Tanzania Government 5½ per cent 1975/79	725,000	689,718/62	90¼	656,125	—	688,757
2. Tanzania Government 6½ per cent 1981/84	400,000	400,000	97	388,000	—	12,000
3. Tanzania Government 6¼ per cent 1980/83	2,000	1,940	94¼	1,885	—	115
4. Tanzania Government 6½ per cent 1969	4,500,000	4,496,490/68	100	4,500,00	—	—
5. Tanzania Government 6½ per cent 1975/78	1,400,000	1,400,000	96¾	1,354,500	—	45,500
6. Tanzania Government 6¾ per cent 1970/71	2,772,000	2,744,280	99	2,761,769	—	10,231
7. Tanzania Government 6½ per cent 1970/71	4,490,000	4,422,650	99¼	4,456,325	—	33,675
8. Tanzania Government 6¾ per cent 1980/81	17,640,100	16,581,694	98½	17,375,497	—	64,603
9. Tanzania Government 6¾ per cent 1983/85	10,985,600	10,656,032	98½	10,779,620	—	205,980
10. Tanzania Government 6 per cent 1972	2,900,000	2,885,500	99¼	2,878,250	—	21,750
11. Tanzania Government 6¼ per cent 1974	2,000,000	2,031,609/60	99¾	1,995,000	—	5,000
12. Tanzania Government 6½ per cent 1987	2,052,000	1,990,440	90	1,859,625	—	192,375
13. Tanzania Government 6 per cent 1975	4,600,000	4,531,000	98	4,508,000	—	92,000
14. Tanzania Government 5¾ per cent 1977	1,800,000	1,773,000	98	1,764,000	—	36,000
15. Zanzibar Government 6½ per cent 1970/72 ...	10,000	100,000	—	—	—	—
16. Tanzania Governnent Development Bonds 5¾ per cent	200,000	200.000	—	—	—	—
17. Treasury Notes 5 per cent 1970	2,170,000	2,148,300	—	—	—	—
Total ...	58,736,700	57,052,654/90	—	57,748,268	—	988,104

Quoted Investments	54,604,354	90
Not Quoted Investments	2,448,300	00
	57,052.654	90

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 1468

AKIBA YA WATUMISHI WA TAWALA ZA MITAA

HESABU ZA AMANA NA MALIPO KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 30.6.1968

1966/1967 Sh.	St.	AMANA	1967/1968 Sh.	St.	1966/1967 Sh.	St.	MALIPO	1967/1968 Sh.	St.
31,577,488	15	Baki ya kutoka nyuma	41,377,837	25	2,541,192	25	Malipo	4,524,632	20
5,436,277	20	Amana zilizopokelewa	5,823,972	50	41,377,837	25	Baki	50,332,571	90
5,436,277	20	Kisutuo	5,823,972	50					
1,468,986	95	Ziada iliyolipwa kwa walimbikaji	1,831,421	85					
43,919,029	50		54,857,204	10	43,919,029	50		54,857,204	10

MAPATO NA MATUMIZI KUFIKIA JUNI, 1968

		MATUMIZI					MAPATO		
38,053	00	Matumizi ya Usimamizi ...	75,421	75	2,066,801	35	Faida	2,898,126	10
1,468,986	95	Ziada iliyolipwa kwa Walimbikaji	1,331,421	85	1,680	00	Faida iliyotokana na kuikomboa Stock 67/68...	2,148	60
21,246	20	Gharama za Benki	14,756	80			Faida ambayo haikupokelewa Tanganyika Stock 1975/78	45,500	00
540,195	20	Mapato yaliyozidi matumizi ...	1,024,174	30					
2,068,481	35		2,945,774	70	2,068,481	35		2,945,774	70

MIZANIA KAMA ILIVOKUWA TAREHE 30.6.1968

		DHIMA					MALI		
41,377,837	25	Baki ya walimbikaji	50,332,571	90	117,508	25	Baki iliyo Benki	70,597	10
933,803	80	Mlimbiko wa Faida	933,803	80					
		Ongeza: mapato yote yaliyozidi matumizi	1,957,978	10			Dhamana zenye bei inayopatikana 30.6.68 Sh. 48,130,179/25 ...	47,268,745	30
					25,808,962	70	Dhamana nyinginezo	2,448,300	00
22,000	20	Deni la Bodi ya Mikopo (L.G.L.B.)			14,655,794	00	Amana na visutuo ambavyo havijalipwa	2,457,407	60
					—		Faida ambayo haijapokelewa ...	45,500	00
					1,666,296	10			
					85,000	00			
					80	00	Deni toka Benki ya Biashara ...		
42,333,641	05		52,290,550	00	42,333,641	05		52,290,550	00

Hesabu za mapato na matumizi pamoja na mizania zilizo hapo juu zimekaguliwa kulingana na yaliyomo katika kifungu cha 3 (6) cha sheria ya Akiba ya Watumishi wa Tawala za Mitaa. Nimepata habari pamoja na maelezo yote niliyohitaji, kwa hiyo ninathibitisha baada ya Ukaguzi huu kwamba, kwa maoni yangu hesabu hizo ni sawa; isipokuwa njia iliyotumiwa kwa kutoa faida inahitilafiana na ile iliyo katika sheria iliyotajwa hapo juu.

S. M. MABEYO
Katibu,
Halmashauri Kuu,
Akiba ya Watumishi wa Tawala za Mitaa

Urban Council Division,
Magogoni Road,
P.O. Box 2400
Dar es Salaam.
6 Oktoba, 72

A. MUSHI,
Mwenyekiti,
Halmashauri Kuu.
Akiba ya Watumishi wa Tawala za Mitaa

M. ABOUD,
Mthibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu

LOCAL AUTHORITY PROVIDENT FUND INVESTMENTS AS AT 30TH JUNE, 1968

STOCK	VALUE					
	Nominal Value (Face Value)	Book Value (Cost Value)	Middle Market	Value as at 30th June, 1968	Appreciation	Depreciation
	Shs. Cts.	Shs. Cts.		Shs. Cts.	Shs. Cts.	Shs. Cts.
Tanganyika Government 5½% stock 1975/79 ...	725,000 00	689,718 62	89½%	648,875 00	—	40,843 62
Tanganyika Government 6½% stock 1981/84 ...	400,000 00	400,000 00	98½%	394,000 00	—	6,00 00
Tanganyika Government 6¼% stock 1980/83 ...	2,000 00	1,940 00	9·5%	1,900 00	—	40 00
Tanganyika Government 6½% stock 1969	4,500,000 00	4,496,490 68	100%	4,500,000 00	3,509 32	—
Tanganyika Government 6½ stock 1975/78	1,400,000 00	1,400,000 00	96½%	1,351,000 00	—	49,000 00
U.R. of Tanganyika & Zanzibar 6¾% stock 1970/71	2,772,000 00	2,744,280 00	99¼%	2,751,210 00	6,930 00	—
Tanganyika Government 6½% stock 1970/71 ...	4,490,000 00	4,422,630 00	99½%	4,467,550 00	44,900 00	—
Tanganyika Government 6¾% stock 1980/81	1,764,100 00	16,581,694 00	98¼%	17,331,398 25	749,704 25	—
U.R. of Tanzania 6¾% stock 1983/85	10,985,600 00	10,656,032 00	98¾%	10,820,816 00	164,784 00	—
Tanzania Government 6% stock 1972	2,900,000 00	2,885,500 00	99¼%	2,878,250 00	—	7,250 00
Tanganyika Government 6¼% stock 1974	1,000,000 00	1,000,000 00	100·5%	1,005,000 00	5,000 00	—
Tanzania Government 6½ stock 1987	2,052,000 00	1,990,440 00	96·5%	1,980,180 00	—	10,260 00
Zanzibar Government 6½ stock 1970/75	100,000 00	100,000 00	—	—	—	—
Tanganyika Government 5¾ Development Bonds ...	200,000 00	200,000 00	—	—	—	—
Treasury Notes 5% 1970	2,170,000 00	2,148,300 00	—	—	—	—
Total ...	51,336,700 00	49,717,045 30		48,130,179 25	974,827 57	113,393 62

LOCAL AUTHORITY PROVIDENT FUND INVESTMENTS AS AT 30TH JUNE, 1968—*(contd.)*

	Shs. Cts.		
Not Quoted	2,448,300 00	48,130,179 25	(Value at 30th June, 1968)
Quoted	47,268,745 30	974.827 57	(Appreciation —Loss)
	49,717,045 30	47,155,351 68	
Total Investiments		113,393 62	Depreciation —Add)
		47,268,745 30	

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 1469

BENKI KUU YA TANZANIA

MIZANIA KAMA ILIVYOKUWA TAREHE 31 AGOSTI, 1972

Dhima		Sh.	*(31.7.72)* *Sh.*
Noti zinazotumika		**1,027,043,405**	*938,256,675*
Sarafu zinazotumika		**95,522,089**	*84,756,651*
Amana:			
Amana za Serikali...	3,043,880		*(7,401,610)*
Amana za Mabenki ya Biashara ...	3,451,114		*(9,091,236)*
Amana nyinginezo...	14,131,894		*(19,740,202)*
		20,626,888	*36,233,048*
Dhima zitokanazo na Nchi za Kigeni		**25,867,020**	*17,440,615*
Mchango wa Tanzania katika Shirika la Ulimwengu la Fedha		**272,131,067**	*272,131,067*
Sehemu ya Tanzania ya Haki maalum ya kuchukua Fedha kutoka Shirika la Ulimwengu la Fedha		**111,068,685**	*111,068,685*
Faida itokanayo na Marekebisho ya Thamani ya Fedha za Nchi za Nje (kufuatana na kifungu cha 15 (3) cha sheria ya Benki ya Tanzania 1965)		**8,370,767**	*8,370,767*
Dhima nyinginezo		**43,420,232**	*43,912,449*
Rasilmali iliyolipwa kwa ukamilifu		**20,000,000**	*20,000,000*
Mlimbuko wa Faida		**32,000,000**	*32,000,000*
	Sh.	**1,656,050,153**	*1,564,169,957*

Mali		Sh.	*(31.7.72)* *Sh.*
MALI ZITOKANAZO NA NCHI ZA KIGENI:			
Fedha za nchi za Kigeni	502,908,820		*(511,688,211)*
Fedha za nchi za Kigeni zitokanazo na Haki maalum ya Tanzania kuchukua fedha kutoka Shirika la Ulimwengu la Fedha ...	52,094,416		*(52,094,416)*
		555,003,236	*563,782,627*
Fungu la Tanzania katika Shirika la Ulimwengu la Fedha		**325,714,899**	*325,714,899*
Dhamana za Serikali:			
Zilizotwaliwa kutoka Halmashauri ya Afrika Mashariki	5,581,161		*(5,581,161)*
Dhamana nyinginezo za Serikali ya Tanzania... ...	356,081,161		*(322,822,514)*
		361,662,322	*328,403,675*
Karadha zilizopewa:			
Serikali	279,000,000		*(260,000,000)*
Mabenki	110,000,000		*(37,000,000)*
		389,000,000	*297,000,000*
Majengo na vifaa		**14,420,501**	*14,276,077*
Malipo yanayokusanywa		**4,298,332**	*27,538,029*
Mali nyinginezo		**5,950,863**	*7,454,650*
	Sh.	**1,656,050,153**	*1,564,169,957*

Dar es Salaam,
16 Septemba, 1972

C. R. MINJA,
Mhasibu Mkuu

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 1470 CI. 5359/111/62

WAHAKIKI WA MADINI WALIOANDIKISHWA

Sheria za Wahakiki wa Madini

(Sura ya 128)

Kwa mujibu wa Ibara ya 11 ya Sheria za Wahakiki wa Madini, inatangazwa kuwa watu wafuatao wameandikikwa katika daftari ya wenye leseni na Wahakiki wa Madini wa Serikali katika Tanzania:—

Wahakiki wa Serikali:

Na. 19.

Jina: AARON ILMARI LESKINEN, M.Sc. (Helsinki), Afisa Uchunguzi.

Anuani: Idara ya Madini, P.O. Box 903, Dodoma.

Tarehe ya kuandikwa: 22 Septemba, 1972.

Maelezo: Kuandikwa chini ya kifungu cha 9 (1) (b) cha Sheria ya Wahakiki wa Madini.

Na. 20.

Jina: BONIFACE JANJUZI MUGYABUSO, B.Sc. (Nairobi), Afisa Uchunguzi.

Anuani: Idara ya Madini, P.O. Box 903, Dodoma.

Tarehe ya kuandikwa: 22 Septemba, 1972.

Maelezo: Kuandikwa chini ya kifungu cha 9 (1) (b) cha Sheria ya Wahakiki wa Madini.

A. O. NASON,
k.n.y. Katibu,
Baraza la Wahakiki wa Madini

Dodoma,
23 Septemba, 1972

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 1471 US/SO/4/IV/B/4

VYAMA VILIVYOANDIKISHWA

Sheria ya Kuandikisha Vyama

(Kifungu cha 337)

(Sharti la 9 la Kuandikisha Vyama)

Taarifa inatolewa kwamba vyama vifuatavyo vimeandikishwa chini ya sehemu ya 7 ya Sheria ya Kuandikisha Vyama.

Nambari	*Jina*
SO. 5789	Christian Booksellers Agency of Tanzania, Dar es Salaam.
SO. 5813	Tanzania Registered Nurses Association, Shinyanga Region Branch, Shinyanga.
SO. 5824	Tanzania Registered Nurses Association, Mara Region Branch, Musoma.
SO. 5825	Tanzania Registered Nurses Association, Iringa Region Branch, Iringa.

Chama kifuatacho kimekataliwa kuandikishwa na Mwandishi wa Vyama chini ya sehemu ya 9 ya Sheria ya Kuandikisha Vyama.

Nambari	*Jina*
SO. 5737	Mozambique African Congress, Dar es Salaam.

Wizara ya Mambo ya Ndani,
Dar es Salaam,
30 Septemba, 1972

E. E. LYIMO,
k.n.y. Mwandishi wa Vyama

(b) Tajiri atatoa ruhusa bila ya kikwazo cho chote kwa mfanyakazi/wafanyakazi wakati wa saa za kazi wanapohitajiwa, ili kuhudhuria mafunzo ambayo mara kwa mara hutayarishwa na Chama, au Shirika lo lote la Taifa au Vyuo vinginevyo.

15. *Matibabu:*

(a) Matibabu yatatolewa bure kwa kila mfanyakazi pamoja na mkewe au mumewe na watoto wake.

(b) Kila mfanyakazi au jamaa yake anapohitaji kwenda kwenye matibabu Tajiri atampa cheti cha matibabu pamoja na chombo cha kusafiria kwenda huko.

16. *Migogoro kazini:*

(i) Migogoro yote itakayotokea kazini, kati ya Tajiri na mfanyakazi kazini ambayo inaweza kushughulikiwa chini ya Sheria ya Usalama Kazini, Na. 62 ya 1964, basi sheria hiyo itatumika kuondoa migogoro hiyo.

(ii) Migogoro au mabishano mengine ambayo hayaji chini ya Sheria Na. 62 ya Usalama Kazini ya mwaka 1964, usuluhishi wake utashughulikiwa kwanza kirafiki, baina ya Kamati ya Kazi kama ipo, na Tajiri ili kufikia uelewano. Iwapo hatua hiyo haitafaulu mgogoro huo utapelekwa kwa Chama kwa kufuata ngazi zake. Ikiwa bado usuluhishi haujapatikana mgogoro huo utafuata Sheria ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi, 1967.

17. *Mpango wa kukuza mazao:*

Chama na Tajiri wamekubaliana kwamba watawafunza wafanyakazi wote juu ya haja na faida ya kukuza utumishi bora na mengine kazini, na kuweka mipango mbali mbali itakayoonekana kuwa itafaa ya kukuza utumishi bora.

18. *Nyongeza za mishahara:*

Imekubaliwa ya kwamba nyongeza za mishahara itakuwa kama ifuatavyo:—

(1) Wafanyakazi 4 wenye mishahara Sh. 185/- hadi Sh. 240/- nyongeza itakuwa Sh. 35/- kwa mwezi kila mmoja.

(2) Wafanyakazi 10 wenye mishahara Sh. 241/- na kuendelea nyongeza itakuwa Sh. 26/- kwa mwezi kila mmoja.

Kwa niaba ya:
United Engineering Works

Partner

Kwa niaba ya:
Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tanganyika (NUTA)

H. C. CHIFUPA,
Katibu wa Tawi

L. W. NGANJI,
Katibu Msaidizi wa Tawi

ROBINSON MOSHI,
Mwenyekiti, Kamati ya Kazi

Dar es Salaam,
28 Februari, 1972

F. L. NYALALI,
Kaimu Mwenyekiti

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 1473

BARAZA LA UAMUZI LA WAFANYAKAZI

Mkataba wa Hiari Na. 10 wa 1972

baina ya

CHAMA CHA TAIFA CHA WAFANYAKAZI TANGANYIKA (NUTA)

na

MATAJIRI WA MAHOTELI, TANGA

Kwa kufuatana na Sheria Na. 41 ya 1967 fungu la 39 kifungu cha 3, mkataba wa hiari baina ya Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tanganyika (NUTA) na Matajiri wa Mahoteli, Tanga, uliletwa mbele ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi (Permanent Labour Tribunal).

Na kutokana na mamlaka yaliyotolewa kwa Baraza hilo kwa mujibu wa Sheria Na. 41 ya 1967 fungu la 39 kifungu cha 7 fasili ya (a) na kwa makubaliano ya pamoja na washauri wa Baraza (Assessors) mkataba ufuatao umekubaliwa kuandikishwa.

Kibali hiki kitaanzia siku ya tarehe 1 Novemba, 1971.

MKATABA WA HIARI

baina ya

CHAMA CHA TAIFA CHA WAFANYAKAZI TANGANYIKA (NUTA)

na

MATAJIRI WA MAHOTELI, TANGA

1. *Makubaliano:*

Sisi Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tanganyika, tujulikanao kwa jina "Chama" na Waajiri wa Mohoteli Mjini Tanga tujulikanao kwa jina "Waajiri", tunathibitisha hapa kwa maandishi na kutia sahihi zetu, kuonyesha kuwa kwa uhuru na hiari yetu wenyewe tumekubaliana juu ya mambo haya yafuatayo kuhusu hali za kazi na mishahara.

2. *Utambuzi:*

(a) Muajiri anakitambua na kuheshimu haki za Chama kuwa ndiye sauti na mtetezi peke yake wa wafanyakazi wote walio wanachama wa NUTA kwa mambo yote yanayohusu hali za kazi na mishahara.

(b) Chama, kwa upande mwingine kinatambua Muajiri kuwa ndiye muajiri peke yake wa wafanykazi wanaohusika na mkataba huu.

3. *Kuhusika:*

(a) Mkataba huu utawahusu wanachama wote wa Chama walioajiriwa na muajiri isipokuwa wale ambao ni wakuu wa kazi.

(b) *Tafsiri ya Mkuu wa kazi:*

Tafsiri ya Mkuu wa kazi itakuwa na maana ifuatayo:—

(i) Mkuu wa Kiwanda; au

(ii) Mkuu wa Kiwanda Masaidizi; au

(iii) Mkuu wa Idara; au

(iv) Mkurugenzi.

Viinginevyo, Mkuu wa kazi, ni mtu ye yote yule aliyepewa madaraka na uwezo kamili kwa maandishi wa kuajiri, kufukuza, na kuachisha kazi mfanyakazi, ama uwezo wa kupendekeza juu ya kuajiri, kumkuza, au kumwachisha kazi mfanyakazi.

4. *Muda na Tarehe ya Kuanza Mkataba:*

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kwamba tarehe ya kuanza mkataba huu itakuwa tarehe 1 Novemba, 1971 na utaendelea kutambuliwa kwa muda usiopungua miezi 12. Katika muda huu, ikiwa ye yote wa pande hizi mbili ana haja ya kubadilisha au kufuta kifungu cho chote cha mkataba huu, ni lazima afuate masharti yaliyomo katika fasili ya 27 (3) ya Sheria ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi (Permanent Labour Tribunal) ya mwaka 1967.

(b) Hata hivyo mkataba unaweza kuvunjwa kwa mkubaliano ya pande zote mbili lakini ye yote katika hao anayetaka kuvunja kifungu cho chote inambidi atoe taarifa ya mwezi mmoja kwa maandishi kwa mwenzake kwa ajili ya kusudio hilo.

(c) Mkataba huu utaendelea kutambuliwa wakati wote mpaka wakati huo tu ambao labda mkataba utavunjwa, au kubadilishwa au kurekebishwa kwa makubaliano ya wote au kwa uamuzi wa Mwenyekiti wa Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi.

5. *Kuajiri:*

Muda wa majaribio utakuwa kama ifuatavyo:

(a) Kwa kazi zisizohitaji ujuzi, mfanyakazi atakuwa kwenye muda wa majaribio ya mwezi mmoja.

(b) Kwa kazi zinazohitaji ujuzi, mfanyakazi atakuwa kwenye muda wa majaribio ya miezi miwili.

(c) Mara baada ya muda wa majaribio kumalizika mfanyakazi atahesabiwa kuwa ni mfanyakazi wa kudumu wa mwezi.

6. *Uachaji au uachishwaji kazi:*

(a) Katika muda wa majaribio upande wo wote:—

(i) Chini ya kifungu 5 (a) utatoa taarifa ya siku moja ya kuacha au kuachishwa kazi au malipo ya fedha badala ya taarifa hiyo.

(ii) Chini ya kifungu 5 (b) utatoa taarifa ya siku 14 ya taarifa ya kuacha au kuachishwa kazi au malipo ya fedha badala yake.

(b) Kuhusu wafanyakazi wa kudumu upande wo wote utatakiwa kutoa taarifa ya mwezi mmoja ya kuacha au kuachishwa kazi au malipo ya fedha badala ya taarifa hiyo. Taarifa hiyo, au malipo badala yake, ni lazima itolewe kwa maandishi.

(c) Mfanyakazi asiachishwe kazi mpaka pamekuwapo na sababu ya maana inayoambatana na uwezo au tabia yake kazini au ustawi wa kazi.

Papo hapo yafuatayo yasiwe ni sababu ya kumwachisha kazi mfanyakazi:—

(i) Kuwa mwanachama wa Chama au kufanya shughuli za Chama nje ya saa za kazi, au wakati wa saa za kazi kwa idhini ya muajiri au msimamizi wake wa kazi.

(ii) Kuwa mjumbe au kiongozi wa wafanyakazi au kugombea kiti cho chote cha ujumbe au uongozi wa wafanyakazi.

(iii) Kutoa malalamiko au kushiriki katika utoaji wa ushahidi juu ya Muajiri kuvunja sheria, kutokufuata siasa ya Taifa au kufanya jambo lo lote la kuwaudhi wafanyakazi.

(iv) Ukabila, rangi, utu, dini, mawazo ya siasa na (Starehe).

7. *Nafasi za kazi na Upunguzaji wafanyakazi:*

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kuwa, juhudi ya pamoja itafanywa ili kuongeza nafasi za kazi na kuzuia upunguzwaji wa wafanyakazi kazini, ili kusaidia Taifa katika kupambana na tatizo la ukosefu wa kazi za mishahara nchini.

(b) Hatua za kuwapunguza idadi ya wafanyakazi, zitachukuliwa tu, iwapo Waajiri watakitosheleza Chama, kuwa hakuna uwezekano wo wote mwingine wa kuepuka au kuzuia hatua hiyo. Hizi zifuatazo zitakuwa miongoni mwa njia zifaazo kufikiriwa juu ya uepukaji wa upunguzaji wafanyakazi; uondoaji wa kazi za ziada; ubadilishaji wa wafanyakazi kutoka sehemu wasikohitajika na kuwaweka kwenye sehemu nyingine ambazo zitaonekana kuwa na nafasi au haja na watu hao; kutoajiri tena, kwa muda, watu wapya mpaka hapo hali itakaporudia tena kuwa njema, upunguzaji wa pole pole kwa wafanyakazi wote watakaohusika.

(c) Uchaguzi wa wafanyakazi watakaohusika na upunguzwaji utafuata msingi wa "Wakwanza kuingia kazini awe wa mwisho kupunguzwa" au kufikiriwa juu ya:—

(a) Hali ya utendaji bora wa kazi za kiwanda.
(b) Uwezo, uzoevu, ujuzi na sifa za kazi za kila mfanyakazi.
(c) Muda wa utumishi.
(d) Umri.
(e) Hali ya jamii yake.

(d) Wafanyakazi ambao wameachishwa kwa ajili ya upunguzwaji, lazima wapewe nafasi ya kwanza ya kurudishwa kazini wakati muajiri anapoajiri wafanyakazi wapya. Kuajiriwa tena kufuate utaratibu uliotajwa hapo juu.

8. *Saa za kazi:*

(a) Saa za kazi zitakuwa 45 kwa juma moja. Jumapili na siku za Sikukuu kwa kawaida hakutakuwa na kazi.

(b) Kazi zo zote zitakazofanyika zaidi ya saa za kazi za kawaida, kwa juma au kwa mwezi zitahesabika kuwa ni kazi za ziada ambazo lazima zitalipwa kwa kiasi cha moja na nusu (1½) cha malipo ya saa za kawaida. Ila tu, ikiwa kazi hizo zitafanyika siku za Jumapili au Sikukuu za Kiserikali, basi malipo yake yatakuwa mara mbili ya kiasi cha malipo ya saa za kawaida.

9. *Ulazima wa uanachama:*

(a) Kila mfanyakazi aliyeajiriwa na muajiri atalazimika kuwa mwanachama wa Chama katika muda wa miezi miwili toka tarehe ya mkataba huu kutangazwa rasmi kwenye *Gazeti* la Serikali.

(b) Mfanyakazi ye yote yule mpya ambaye atakayeajiriwa atalazimika kuwa mwanachama wa Chama katika muda wa miezi 2 mara baada ya kumaliza muda wake wa majaribio. Au ikiwa hatahusika na muda wa majaribio, atalazimika kuwa mwanachama wa Chama katika muda wa miezi miwli toka ameajiriwa.

(c) Mfanyakazi ye yote ambaye hatakuwa mwanachama wa Chama kwa mujibu wa Ibara hii atakuwa ametoa taarifa yake ya kuacha kazi.

10. *Nguo na au vifaa vya kuhifadhi mwili kazini:*

(a) Wafanyakazi wenye daraja hizi zifuatazo hapa chini watapewa jozi mbili za nguo kwa mwaka na vifaa vya kuhifadhi mwili:—

1. Wapishi.
2. Waandazi (Waiters).
3. Waangalizi wa hoteli (Hotel Attendances).

(b) Wafanyakazi wote ambao wamepewa nguo na vifaa vya kuhifadhi miili itawalazimu kuvivaa katika nyakati zote za saa za kazi.

11. *Ada za NUTA:*

Imekubaliwa kwamba Muajiri atakuwa anakata ada za NUTA kila mwezi kutokana na mshahara wa kila mfanyakazi ambaye ni mwanachama wa NUTA na kuzituma pesa hizo kwenye Makao Makuu ya NUTA kupitia Mahesabu Na. 1 huko katika Tawi la Benki ya Taifa ya Biashara, Mtaa wa Market, Dar es Salaam.

12. *Marupurupu:*

Mambo yote yaliyotajwa hapa chini yatalipwa na muajiri kwa mujibu wa "Sheria ya Marupurupu ya 1968":—

(1) Likizo ya mwaka na malipo yake.
(2) Likizo ya ugonjwa na malipo yake.
(3) Likizo ya uzazi.
(4) Likizo ya ugonjwa wa uzazi na malipo yake.
(5) Likizo ya dharura.
(6) Malipo ya safari ya likizo.

13. *Mpango wa mafunzo kwa wafanyakazi:*

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kwamba wafanyakazi wanastahili kupewa mafunzo zaidi juu ya kazi yao, ili waweze kutoa utumishi/mazao mengi na bora zaidi. Kwa ajili hiyo muajiri, ataweka mpango maalum wa mafunzo kwa wafanyakazi.

(b) Muajiri atatoa ruhusa bila ya kikwazo cho chote kwa mfanyakazi/wafanyakazi, wakati wa saa za kazi inapohitajiwa, ili wahudhurie mafunzo ambayo mara kwa mara hutayarishwa na Chama, au Shirika lo lote la Taifa au vyuo vinginevyo.

14. *Matibabu:*

(a) Matibabu yatatolewa bure kwa kila mfanyakazi.

(b) Kila mfanyakazi anapohitaji kwenda katika matibabu tajiri atampa cheti cha matibabu.

15. *Migogoro kazini:*

(i) Migogoro yote itakayotokea kazini, kati ya muajiri na mfanyakazi kazini ambayo inaweza kushughulikiwa chini ya Sheria ya Usalama Kazini, Namba 62 ya mwaka 1964, basi sheria hiyo itatumiwa kuondoa migogoro hiyo.

(ii) Migogoro au mabishano mengine ambayo hayaji chini ya Sheria Namba 62 ya Usalama Kazini ya mawka 1964, usuluhishi wake utashughulikiwa kwanza kirafiki, baina ya Kamati ya Kazi kama ipo, na tajiri ili kufikia uelewano. Iwapo hatua hiyo haitafaulu mgogoro huo utapelekwa kwa Chama kwa kufuata ngazi zake. Ikiwa bado usuluhishi haujapatikana, mgogoro huo utafuata Sheria ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi 1967.

16. *Mpango wa kukuza mazao:*

Chama na muajiri wamekubaliana kwamba watawafunza wafanyakazi wote juu ya haja na faida ya kukuza utumishi/mazao bora na mengine kazini, na kuweka mipango mbali mbali itakayoonekana kuwa itafaa ya kukuza utumishi/mazao mengi na bora. Mipango hiyo itakuwa na mkataba wake maalum.

17. *Nyongeza ya mishahara:*

Imekubaliwa ya kwamba nyongeza za mishahara zitakuwa kama hivi ifuatavyo hapa chini.—

Daraja	*Wafanyakazi*	*Mshahara*	*Nyongeza*
(i)	50	Sh. 170/- hadi Sh 250/-	Sh. 15/-
(ii)	20	Sh. 251/- na zaidi	Sh. 10/-

Mkataba huu umetiwa sahihi siku ya Jumanne, tarehe 19 Oktoba, 1971.

Kwa niaba ya:
Wenye Mahoteli, Tanga

1. Bismilah Hoteli
2. Muna Hoteli
3. Township Hoteli
4. Safari Hoteli
5. New Lux Hoteli
6. Kigoma Hoteli
7. Muungano Hoteli
8. Country Hoteli
9. Zam Zam Hoteli
10. Dunia Hoteli
11. Kilimanjaro Hoteli
12. Tanga Hoteli
13. Keto Hoteli
14. Harambee Hoteli
15. Zanzibar Hoteli
16. Taifa Hoteli

Kwa niaba ya:
Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tanganyika (NUTA)

A. A. Mwinyigoha,
Katibu wa Tawi

M. Sadiki,
Katibu Msaidizi wa Tawi

Salehe Mawji,
Mjumbe wa Kamati ya Kazi

Ahemed Ali,
Mjumbe wa Kamati ya Kazi

Dar es Salaam,
26 Februari, 1972

F. L. Nyalali,
Kaimu Mwenyekiti

Taarifa ya Kawaida Na. 1474

BARAZA LA UAMUZI LA WAFANYAKAZI

Mkataba wa Hiari Na. 224 wa 1971

baina ya

CHAMA CHA TAIFA CHA WAFANYAKAZI TANGANYIKA (NUTA)

na

MPWAPWA CATHOLIC MISSION

Kwa kufuatana na Sheria Na. 41 ya 1967 fungu la 39 kifungu cha 3, mkataba wa hiari baina ya Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tanganyika (NUTA) na Roman Catholic Mission, Mpwapwa uliletwa mbele ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi (Permanent Labour Tribunal).

Na kutokana na mamlaka yaliyotolewa kwa Baraza hilo kwa mujibu wa Sheria Na. 41 ya 1967 fungu la 39 kifungu cha 7 fasili ya (a) na kwa makubaliano ya pamoja na washauri wa Baraza (Assessors) mkataba ufuatao umekubaliwa kuandikishwa.

Kibali hiki kitaanzia siku ya tarehe 1 Oktoba, 1971.

Mkataba wa Hiari

baina ya

Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tanganyika (NUTA)

na

Roman Catholic Mission

1. *Makubaliano:*

Sisi Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tanganyika, tujulikanao hapa kwa jina "Chama" na Mission Catholic ya Mpwapwa tujulikanao kwa jina "Mwajiri", tunathibitisha hapa kwa maandishi na kutia sahihi zetu, kuonyesha kuwa, kwa hiari yetu wenyewe, tumekubaliana juu ya mambo haya yafuatayo kuhusu hali za kazi na mishahara.

2. *Utambuzi:*

(a) Mwajiri anakitambua na kuheshimu haki za Chama, kuwa ndiye mtetezi peke yake wa wafanyakazi wote walio wanachama wa NUTA kwa mambo yote yanayohusu hali za kazi na mishahara.

(b) Chama, kwa upande mwingine kinatambua Mwajiri, kuwa ndiye Mwajiri peke yake wa wafanyakazi wanaohusika na mkataba huu.

3. *Muda na tarehe ya kuanza mkataba:*

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kwamba, tarehe ya kuanza mkataba huu, itakuwa 1 Oktoba, 1971 na utaendelea kutambuliwa kwa muda usiopungua miezi 12. Katika muda huu, ikiwa ye yote wa pande hizi mbili ana haja ya kubadilisha au kufuta kifungu cho chote cha mkataba huu, ni lazima afuate masharti yaliyomo katika ibara ya 27 (3) ya Sheria ya Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi (Permanent Labour Tribunal) ya mwaka 1967.

(b) Hata hivyo mkataba unaweza kuvunjwa kwa makubaliano ya pande zote mbili, lakini ye yote katika hao anayetaka kuvunja kifungu cho chote inambidi atoe taarifa ya mwezi mmoja kwa maandishi, kwa mwenzake kwa ajili ya kusudio hilo. Mkataba huu utaendelea kutambuliwa wakati wote mpaka utakapovunjwa au kubadilishwa kwa au kurekebishwa kwa makubaliano ya wote au kwa uamuzi wa Mwenyekiti wa Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi.

4. *Kuajiri:*

Muda wa majaribio utakuwa kama ifuatavyo:—

(a) Kwa kazi zisizohitaji ujuzi, mfanyakazi atakuwa kwenye majaribio ya mwezi mmoja.

(b) Mara baada ya muda wa majaribio kumalizika, mfanyakazi atahesabiwa kuwa ni mfanyakazi wa kudumu na mshahara wake utalipwa kwa mwezi.

5. *Uachaji au uachishwaji kazi:*

Katika muda wa majaribio, upande wo wote utalazimika:—

(a) Chini ya kifungu 4 (a) kutoa taarifa ya siku 14 ya kuacha au kuachishwa kazi au malipo ya fedha badala yake.

(b) Kuhusu wafanyakazi wa kudumu, upande wo wote utatakiwa kutoa taarifa ya mwezi mmoja ya kuacha au kuachishwa kazi au malipo ya fedha ya mwezi mmoja badala ya taarifa hiyo. Taarifa hiyo au malipo badala yake, ni lazima itolewe kwa maandishi.

(c) Mfanyakazi asiachishwe kazi mpaka pamekuwepo na sababu ya maana inayoambatana na uwezo au tabia yake kazini au ustawi wa kazi. Papo hapo yafuatayo yasiwe ni sababu ya kumwachisha kazi:—

(i) Kuwa mwanachama wa NUTA au kufanya shughuli za Chama nje ya saa za kazi, au wakati wa saa za kazi kwa idhini ya Tajiri au msimamizi wake wa kazi.

(ii) Kuwa mjumbe au kiongozi wa wafanyakazi au kugombea kiti cho chote cha ujumbe au uongozi wa wafanyakazi au Chama cho chote cha Siasa au Starehe.

(iii) Kutoa malalamiko au kushiriki katika utoaji wa ushahidi juu ya Mwajiri kuvunja sheria, kutokufuata Siasa ya Taifa au kufanya jambo lo lote la kuwaudhi wafanyakazi.

(iv) Ukabila, rangi, utu, dini, mawazo ya siasa na (Starehe).

6. *Nafasi za kazi na upunguzaji wafanyakazi:*

(a) Pande zote mbili zimekubaliana kuwa, juhudi ya pamoja itafanywa ili kuongeza nafasi za kazi na kuzuia upunguzaji wa wafanyakazi kazini, ili kusaidia Taifa katika kupambana na tatizo la ukosefu wa kazi za mishahara nchini.

(b) Hatua za kupunguza idadi ya wafanyakazi, zitachukuliwa tu, iwapo Mwajiri atakitosheleza Chama, kuwa hakuna uwezekano wo wote mwingine wa kuepuka au kuzuia hatua hiyo. Hizi zifuatazo zitakuwa miongoni mwa njia zifaazo kufikiriwa juu ya uepukaji wa upunguzaji wafanyakazi; uondoaji wa kazi za ziada; ubadilishaji wa wafanyakazi kutoka sehemu wasikohitajika na kuwaweka kwenye

sehemu nyingine ambazo zitaonekana kuwa na nafasi au haja na watu hao. Kutoajiri tena, kwa muda watu wapya mpaka hapo hali itakaporudia tena kuwa njema; upunguzaji wa pole pole kwa wafanyakazi wote watakohusika.

(c) Uchaguzi wa wafanyakazi watakaohusika na upunguzwaji utafuata msingi wa "Wakwanza kuingia kazini awe wa mwisho kupunguzwa, na mwisho kuingia kazini atakuwa wa kwanza kupunguzwa".

Pia mambo yafuatayo hapa nayo yatafikiriwa:—
(a) Haja ya utendaji bora wa kazi.
(b) Uwezo, ujuzi na sifa za kazi.
(c) Umri.
(d) Hali ya jamii yake.

(d) Wafanyakazi ambao wameachishwa kwa ajili ya upunguzaji lazima wapewe nafasi ya kwanza ya kurudishwa kazini wakati nafasi za kazi zitakapotokea tena.

7. *Saa za kazi:*

(a) Saa za kazi zitakuwa 45 kwa juma. Jumapili na siku za Sikukuu kwa kawaida hakutakuwa na kazi.

(b) Kazi zo zote zitakazofanyika zaidi ya saa za kawaida kwa juma au mwezi zitahesabika kuwa ni kazi za ziada ambazo lazima zitalipwa kwa kasi cha 1½ (moja na nusu) ya malipo ya saa za kawaida. Ila tu ikiwa kazi hizo zitafanyika siku za Jumapili au Sikukuu za Kiserikali, basi malipo yake yatakuwa mara mbili ya kiasi cha malipo ya saa za kawaida.

8. *Ulazima wa uanachama:*

(a) Kila mfanyakazi aliyeajiriwa na Mwajiri atalazimika kuwa mwanachama wa NUTA, katika muda wa miezi miwili toka tarehe ya kuanza kwa mkataba huu.

(b) Mfanyakazi ye yote mpya, atakayeajiriwa, atalazimika kuwa mwanachama wa NUTA katika muda wa miezi 2 mara baada ya kumaliza muda wake wa majaribio.

(c) Mfanyakazi ye yote ambaye hatakuwa mwanachama wa NUTA kwa mujibu wa fasili (b) ya Ibara hii atahesabika kuwa amejitoa kazi yeye mwenyewe.

9. *Nguo na vifaa vya kuhifadhi mwili kazini:*

(a) Wafanyakazi wenye daraja hizi zifuatazo hapa chini watapewa jozi mbili za nguo na vifaa vya kuhifadhi mwili kwa mwaka:—

Waseremala.
Walehemiaji.
Makanika.

(b) Wafanyakazi wote ambao wamepewa nguo na vifaa vya kuhifadhi miili yao, itawalazimu kuvivaa nyakati zote za kazi.

10. *Ada za NUTA:*

Imekubaliwa kwamba Muajiri atakuwa anakata ada za NUTA kila mwezi kutokana na mshahara wa kila mfanyakazi ambaye ni mwanachama wa NUTA na kuzituma pesa hizo kwenye Makao Makuu ya NUTA, Dad es Salaam au kupitia Mahesabu Na. 1, katika Tawi la Benki ya Biashara, Mtaa wa Market, Dar es Salaam.

11. *Marupurupu ya wafanyakazi:*

Pande zote mbili, Chama na Mwajiri, tumekubaliana kuendelea na likizo ya hivi sasa, ya siku 21, yenye malipo kamili. Isipokuwa utaratibu wa kwenda likizoni utafuatana na ule uliotolewa na Tangazo la Serikali la tarehe 30 Desemba, 1968, kuhusu marupurupu. Mengine yote yafuatayo hapa chini yatafuata sheria hiyo ya marupurupu kwa mujibu wa tangazo la mwezi Desemba, 1968.

Utaratibu wa mapumziko ya likizo watumishi kati ya miaka 1–3 mapumziko ya siku 12.

Kati ya miaka 4–6 mapumziko ya siku 15.
Kati ya miaka 7 au zaidi mapumziko siku 18.

Tofauti kati ya siku 21 na siku za mapumziko Mwajiri atalipa fedha taslimu badala ya mapumziko.

(i) Likizo ya ugonjwa na malipo yake.
(ii) Likizo ya uzazi.
(iii) Likizo ya ugonjwa baada ya uzazi na malipo yake.
(iv) Likzo ya dharura.
(v) Malpo ya safari ya likizo.

12. *Matibabu:*

(a) Kwa vile matibabu ni jambo la muhimu katika kulinda afya ya binadamu, na kwa kuwa saa nyingi za kazi hutumiwa na wafanyakazi, kwa ajili ya kujipatia matibabu mahali mbali na pale pa kazi, au kwa sababu ya upungufu wa utumishi wa hospitali, Mwajiri atafanya mpango wa kuleta matibabu kiwandani mwake, kwa kuajiri Daktari wa muda yeye mwenyewe au kwa kushirikiana na matajiri wengine au kwa kuweka utaratibu mwingine wa kufaa zaidi.

(b) Matibabu yatatolewa bure kwa kila mfanyakazi pamoja na jamii yake.

(c) Kila mfanyakazi au jamii yake anapohitaji kwenda kwenye matibabu Mwajiri atampa cheti cha matibabu.

13. *Migogoro kazini:*

(i) Migogoro yote itakayotokea kazini kati ya Mwajiri na mfanyakazi ye yote ambayo inaweza kushughulikiwa chini ya Sheria ya Usalama Kazini Na. 62 ya 1964 basi, sheria hiyo itatumiwa kuondoa migogoro hiyo.

(ii) Migogoro au mabishano ambayo hayaji chini ya Sheria Na. 62 ya Usalama Kazini ya mwaka 1964, usuluhishi wake utashughulikiwa kwanza kirafiki baina ya Kamati ya kazi na Tajiri ili kufikia uelewano. Iwapo hatua hiyo haitafaulu, mgogoro huo utapelekwa kwa NUTA, kwa kufuata ngazi zake. Ikiwa bado haujapatikana usuluhishi mgogoro huo utapelekwa kwenye Baraza la Uamuzi la Wafanyakazi.

14. *Mpango wa mafunzo ya kazi na ufanisi wa kazi:*

Mpango wa Mwajiri tumekubaliana kwamba tutawafunza wafanyakazi wote juu ya haja na faida ya kukuza utumishi bora kazini, na kuweka mipango mbali mbali itakayoonekana kuwa itafaa kukuza utumishi bora. Kwa hivi sasa Mwajiri yumo mbioni. Katika mipango ya kuanzisha shule ya Useremala, ili kuwasaidia wafanyakazi wake pamoja na vijana wapendao mafunzo hayo toka Vijijini vya Ujamaa vilivyo jirani.

15. *Nyongeza ya mshahara:*

Mwajiri na Chama tumekubaliana kwamba nyongeza za mishahara zitakuwa kama hivi ifuatavyo:—

Daraja	Idadi ya Wafanyakazi	Mshahara wa Zamani	Nyongeza ya Mshahara	Mshahara Mpya	Jumla ya Nyongeza kwa mwezi
I	4	160/— 182/-	16/-	176/— 198/—	64/-
II...	10	210/— 240/-	14/-	224/— 254/-	140/-
III	5	256/— 300/-	13/-	269/— 313/-	65/-
IV	1	400/-	10/20	410/20	10/20
					279/20

Mkataba huu umetiwa sahihi siku ya Alhamisi, tarehe 7 Oktoba, 1971.

Kwa niaba ya:
Mpwapwa Catholic Mission

Bruda FRANCIS, O.F.M. CAP.,

Padre LEONARD, O.F.M. CAP,

Kwa niaba ya:
Chama cha Taifa cha Wafanyakazi Tanganyika (NUTA)

G. M. MANYONYI,
Katibu wa Mkoa

B. A. KITENGA,
Katibu Msaidizi wa Tawi

L. U. C. PALAHANI,
Afisa Uhandisi na Tija Viwandani, Makao Makuu ya NUTA, Dar es Salaam

S. N. ZIMPUNGULU,
Mwenyekiti wa Kamati ya Kazi

Dar es Salaam,
28 Februari, 1972

F. L. NYALALI,
Kaimu Mwenyekiti

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 1475 LD. 56843

UBATILISHO WA HAKI YA KUMILIKI ARDHI

Hati ya Haki ya Kumiliki Ardhi yenye *Land Office No. 20037, Certificate of Title No. 14397* juu ya Kiwanja Na. 70, Kitalu "K", Babati, ambayo ilimilikiwa na SULEMAN JIVRAJ ilibatilishwa kwa mamlaka ya Mtukufu Rais mnamo tarehe 31 Agosti, 1972.

Dar es Salaam,
3 Oktoba, 1972

K. S. LUGAKINGIRA,
Kamishna wa Ardhi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 1476 BS/O. 20/8/105

KUPOTEA KWA KITABU CHA KUAGIZIA VIFAA
(LOCAL PURCHASE ORDER)
(NA. 262901–262950)

Kitabu hicho ambacho Nambari 2629027–262950 hakijatumika bado kimepotea huko Monduli katika Ofisi ya Takwimu, tarehe 3 Septemba, 1972.

Kuanzia tarehe hiyo basi, matumizi ya kitabu hicho si halali. Mtu ye yote atakayekiona au kuona karatasi ya kitabu hicho anaombwa atoe taarifa kwenye Kituo cha Polisi au kwa mwenye kutoa tangazo hili mara moja.

Takwimu,
P.O. Box 796,
Dar es Salaam,
3 Oktoba, 1972

J. A. A. MTIMA,
k.n.y. Mkurugenzi wa Takwimu

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 1477

KUPOTEA KWA HATI YA BIMA

NATIONAL INSURANCE CORPORATION OF TANZANIA LIMITED
(SHIRIKA LA BIMA YA TAIFA)

HATI NA. L/66/2561 JUU YA MAISHA YA BWANA STEPHEN NEEMA

Taarifa imetolewa kuhusu kupotea hati ya bima iliyotajwa hapo juu, nakala yake itatolewa kama malalamiko kupinga kutolewa kwa hati hiyo hayakuwakilishwa kwenye Shirika hili mwezi mmoja kuanzia tarehe ya tangazo hili.

Dar es Salaam,
30 Septemba, 1972

S. KRISHNAMURTHY,
k.n.y. Meneja Mkuu

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 1478

KUPOTEA KWA POLICY

PAN AFRICA INSURANCE COMPANY LIMITED
(Incorporated in Kenya)
MOMBASA

POLICY NO. 14449 YA SH. 20,000/- YA MAISHA YA BWANA BASHIRI ABDALLAH SALIM, P.O. BOX 272, ARUSHA, TANZANIA

Baada ya ilani kutolewa kutokana na upoteaji wa *Policy* iliyotajwa hapo juu, nakili yake itatolewa isipokuwa kuwe na pingamizi ambalo litajulishwa aliyeweka sahihi chini kwa muda wa mwezi mmoja kutoka tarehe ya leo.

P.O. Box 90383,
Mombasa,
27 Septemba, 1972

M. D. NAVARE,
Executive Director

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 1479 Z/D/3

MAOMBI YA LESENI ZA MAGARI YA ABIRIA, UCHUKUZI WA MIZIGO NA MABADILIKO YA LESENI

Kutokana na kifungu cha Sheria za Umilikaji wa Leseni ya mwaka 1958, inakujulisha ya kwamba, utaratibu kama ulivyopangwa katika orodha ya leseni kama ifuatavyo:—

Mtu ye yote anayehusika na kifungu cha Sheria za Usafirishaji na ambaye angependa kupinga katika maombi haya apeleke maombi ya kupinga katika Baraza la Utoaji Leseni za Usafirishaji, S.L.P. 1910, Dar es Salaam. Maombi haya yafike katika Baraza hili (Transport Licensing Authority) kabla ya tarehe 27 Oktoba, 1972. Maombi yote ya aina hiyo yawe kama vile ilivyoonyeshwa katika fungu la pili la masahihisho ya Sheria za Leseni za Usafirishaji mwaka 1963. Nakala za fomu za aina hiyo zinapatikana katika Ofisi za Internal Revenue Officers.

ORODHA

(Angalia: **R.S.L. = Leseni za Magari ya Abiria.**
P.C.L. = Leseni za Magari ya Usafirishaji wa Mizigo).

DO/2462—Coast Region Transport Co. Society Ltd., S.L.P. 15529, Dar es Salaam. Ombi la kuongeza (i) magari matatu ya abiria 67 kila moja na (ii) njia (a) Sekenke mpaka Singida kupitia Itemo na Iguguno na (ii) Isanzu mpaka Singida kupitia Mkalamo, Nduguti na Iguguno na (iii) Lambi mpaka Singida kupitia Singa na Ilongero. (352)

2463—Wella Bus Services, S.L.P. 29, Singida. Ombi la kuongeza gari moja la abiria 45 katika njia ya kutoka Sepuka mpaka Singida (mara tatu kwa siku). Leseni ya sasa: angalia ombi Nambari DO/2354. (177)

2464—Hemedi Salim, c/o Kolo Primary Court, S.L.P. 36, Kondoa Irangi. Ombi la leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 30 katika njia ya kutoka Makafa mpaka Kondoa kupitia Bereko, Ororimo, Suera, Thawi, Kolo na Bolisa.

2465—Salimu Chundu, S.L.P. 36, Kilema. Ombi la leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 50 katika njia ya kwenda kwenye minada katika Wilaya ya Kondoa.

2467—Kilimanjaro Bus Service (1967) Ltd., S.L.P. 361, Arusha. Ombi la kuongeza njia ya kutoka Moshi mpaka Mbeya kupitia Dodoma. Leseni ya sasa: angalia ombi Nambari MS/3238. (161/AR)

2468—Ali Isaka, S.L.P. 312, Dodoma. Ombi la leseni ya mizigo kwa gari moja la tani 7 katika barabara za Mikoa ya Dodoma, Singida na Arusha.

2469—Kassim Ramadhani, S.L.P. 113, Korogwe. Ombi la leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 55 katika njia ya kutoka Dodoma mpaka Korogwe kupitia Dosidosi, Kibaya, Mgera na Handeni.

2470—Haruun Idi Taratibu, S.L.P. 411, Dodoma. Ombi la kuendeleza leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 55 katika njia ya kutoka Dodoma mpaka Mloa kupitia Matumbulu, Nkulabi, Mbasha, Maziwa na Ntintu, kama ilivyo leseni ya sasa. (140)

2471—Ramadhani Ali, S.L.P. 36, Kondoa. Ombi la leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 26 katika njia ya kutoka Kondoa mpaka Mrijo kupitia Kibaya.

2472—Y. M. Mgale, M. Ndalu na H. A. Noor, S.L.P. 91, Manyoni. Ombi la kuendeleza leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 56 katika njia ya kutoka Kwamtoro mpaka Ikasa kupitia Sanzawa, Makanda, Kintinku, Chikuyu na Makusuko, kama ilivyo leseni ya sasa. (66)

2473—Ladhu Moledina Shah, S.L.P. 3, Dodoma. Ombi la leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 55 katika njia ya kutoka Dodoma mpaka Dosidosi kupitia Kongwa, Segele na Mkutani (kwa siku za Jumatatu na Alhamisi) na Hogoro (kwa siku za Jumanne, Jumatano na Jumapili). (15)

2474—Mabwana Salim Kimolo na Harry Bakari, S.L.P. 64, Kondoa. Ombi la kuendeleza leseni ya mizigo kwa gari moja la tani 10 katika barabara za Mikoa ya Dodoma na Singida na barabara ya kwenda (i) Moshi kupitia Arusha na (ii) Dar es Salaam kupitia Morogoro, kama ilivyo leseni ya sasa. (70)

2475—Hassanali Hassam Dewji, S.L.P. 3, Singida. Ombi la kuongeza gari moja la abiria 60 katika njia ya kutoka Sepuka mpaka Singida. Leseni ya sasa: angalia ombi Na. DO/2046. (83)

2476—Hassanali Hassam Dewji, S.L.P. 3, Singida. Ombi la kuongeza gari moja la abiria 60 katika njia ya kutoka Itigi mpaka Singida. Leseni ya sasa: angalia ombi Na. DO/2046. (83)

2477—T. H. Fancy, S.L.P. 12, Singida. Ombi la leseni ya mizigo kwa gari moja la tani 7 na gari moja la tani 6 katika barabara za Mkoa wa Singida na barabara ya kwenda Nzega na Shinyanga.

2478—Furia Ndesuo Massawe, S.L.P. 221, Dodoma. Ombi la leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 55 katika njia ya kutoka Dabalo mpaka Dodoma kupitia Msanga.

2479—Francis Mumbee, S.L.P. 124, Singida. Ombi la leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 26 katika njia ya kutoka Singida mpaka Merya kupitia Ilongera.

2480—Mohamedali Kassam Abji, S.L.P. 253, Dodoma. Ombi la kuendeleza leseni ya mizigo kwa gari moja la tani 5 katika barabara za Mikoa ya Dodoma na Singida, kama ilivyo leseni ya sasa.

LD/4199—Simon Poliforp, S.L.P. 56, Lindi. Ombi la kuendeleza leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 35 katika njia ya kutoka Lindi mpaka Narung'ombe kupitia Mtama, Mnacho, Mkowe na Ruangwa, kama ilivyo leseni ya sasa. (87)

4200—Hassani Mohamed Makuti & Co., S.L.P. 146, Lindi. Ombi la leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 40, gari moja la abiria 52 na gari moja la abiria 48 katika njia ya kutoka Mahurunga mpaka Mtwara kupitia Mbwala, Nanguruwe na Kitaya. (84)

4201—Jaffery's Express Transport Service, S.L.P. 186, Lindi. Ombi la leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 60 katika njia ya kutoka Lindi mpaka Dar es Salaam kupitia Nangurukuru na Rufiji.

4202—Hamisi Seif Manyarasoko, S.L.P. 506, Mtwara. Ombi la kuendeleza leseni ya mizigo kwa gari moja la tani 7 katika barabara za Mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma na katika barabara ya kwenda Dar es Salaam kupitia Kilwa. Leseni ya sasa: gari moja la tani 7 katika barabara za Mikoa ya Mtwara na Ruvuma. (103)

4203—Ramadhani S. Petters, Muhubu Jaffu & Dadi Napelekela, S.L.P. 54, Newala. Ombi la leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 65 katika njia ya kutoka Newala mpaka Dar es Salaam kupitia Lindi, Kilwa, Nangurukuru, Muhoro, Kibiti na Mkuranga.

4204—Issa Saidi, S.L.P. 18, Lindi. Ombi la leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 51 katika njia ya kutoka Lindi mpaka Dar es Salaam kupitia Nangurukuru na Mohoro.

4205—Tanzania Service Company, S.L.P. 123, Mtwara. Ombi la kuendeleza leseni ya mizigo kwa magari manne ya tani 9 katika barabara za Dar es Salaam mpaka Mtwara kupitia Morogoro, Iringa, Njombe, Songea na Tunduru, kama ilivyo leseni iliyomalizika. (19)

4206—Tatu Shah & Turiki Mohamed, S.L.P. 45, Nachingwea. Ombi la leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 56 katika njia ya kutoka Mnero Mission mpaka Lindi kupitia Nachingwea, Nanganga, Mtama na Mingoyo. (41)

4207—Tatu Shah & Turiki Mohamed, S.L.P. 45, Nachingwea. Ombi la kuongeza njia ya kutoka Lindi mpaka Dar es Salaam kupitia Kilwa Kivinje na Mohoro. Leseni ya sasa: angalia ombi Nambari LD/4098.

4208—Hassan Ali Walji, S.L.P. 51, Mtwara. Ombi la leseni ya mizigo kwa gari moja la tani 1½ katika barabara za Mikoa ya Mtwara na Lindi.

MZ/5792—Chotu Thakarar, S.L.P. 82, Musoma. Ombi la kuendeleza leseni ya mizigo kwa gari moja la tani 6 katika barabara za Mkoa wa Mara, kama ilivyo leseni ya sasa. (217)

5793—Khamisi Mohamed, S.L.P. 1016, Bunda. Ombi la leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 59 katika njia ya kutoka Bunda mpaka Shirati kupitia Makutano, Utegi na Shirati. (64)

5794—Khamisi Mohamed, S.L.P. 1016, Bunda. Ombi la leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 59 katika njia ya kutoka Bunda mpaka Mugumu kupitia Ikizu na Nata. (64)

5795—Messrs. Mohamed Hemed & Cosmas Keya, S.L.P. 269, Shinyanga. Ombi la leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 32 katika njia ya kutoka Shinyanga mpaka Usombo kupitia Old Shinyanga, Sayu, Mwangosha na Kijiji cha Ujamaa Kwakaranga.

5796—Messrs. Marinus Atendo Odingo & Bros., S.L.P. 124, Tarime. Ombi la leseni ya abiria kwa magari mawili ya abiria 72 katika njia ya kutoka Tarime mpaka Shirati kupitia Sirari, Bugire, Maumau na Nyambori. (108)

5797—Machibya Seni, S.L.P. 138, Shinyanga. Ombi la kuendeleza leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 45 katika njia ya kutoka Shinyanga mpaka Bariati kupitia Nkolandoto, Mwadui, Mondo na Maswa, kama ilivyo leseni ya sasa. (253)

5798—Elifuraha E. Mrema, S.L.P. 1659, Mwanza. Ombi la leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 27 katika njia ya kutoka Bukumbi Ginnery mpaka Mwanza kupitia Ginnery, Kigongo, Bukumbi Hospital, Usagara, Mkolani na Mkuyuni. (32)

5799—Elifuraha E. Mrema, S.L.P. 1659, Mwanza. Ombi la leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 52 katika njia ya kutoka Ngudu mpaka Mwanza kupitia Chamera, Chapakuna, Ujingwa, Masuha, Sumve, Ishingisha, Koromije, Kanyerere na Kisesa. (32)

5800—Rashid Suleman, S.L.P. 1015, Bunda. Ombi la kuongeza njia ya kutoka Saragana mpaka Masanza, Kahasa, Bunda na Nassa (kwenda na kurudi). (120)

5801—Rashid Suleman, S.L.P. 1015, Bunda. Ombi la kuongeza njia ya kutoka Kisorya mpaka Mugumu kupitia Bunda, Ikizu, Mugeta na Isenye (kwenda na kurudi). (120)

MZ/5802—Rashid Suleman, S.L.P. 1015, Bunda. Ombi la kuongeza njia ya kutoka Bariati mpaka Bunda kupitia Nyakabindi, Dutwa, Ngasama na Mkura (kwenda na kurudi). (120)

5803—Seif Mohamed, S.L.P. 1015, Bunda. Ombi la leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 55 katika njia ya kutoka Musoma mpaka Bunda kupitia Kiabakari na Mwibagi.

5804—Seif Mohamed, S.L.P. 1015, Bunda. Ombi la leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 72 katika njia ya kutoka Mugumu mpaka Mwanza kupitia Mugeta, Ikizu, Bunda na Nasa. (MZ/5803)

5805—Jackson Mugaya Mwita, S.L.P. 313, Musoma. Ombi la leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 63 katika njia ya kutoka Kisaka-Musoma-Busawe-Majimoto-Silorisimbo-Kiagata-Makutano. (190)

5806—Jackson Mugaya Mwita, S.L.P. 313, Musoma. Ombi la leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 54 katika njia ya kutoka Musoma-Bisawe-Makutano-Kiagata-Sirolisombo-Majimoto. (190)

5807—Lucas Kitugi Nungu, S.L.P. 235, Musoma. Ombi la kuendeleza leseni ya mizigo kwa gari moja la tani 7 katika barabara za Mkoa wa Mara, kama ilivyo leseni ya sasa. (258)

5808—Hamud Suleman, S.L.P. 36, Shinyanga. Ombi la leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 62 katika njia ya kutoka Sheluwe mpaka Shinyanga kupitia Igunga, Kininginira, Masanga, Shagihiru, Mhunze na Ukenyenge.

5809—Ally Mohamed, S.L.P. 105, Musoma. Ombi la kuendeleza leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 56 na gari moja la abiria 67 katika njia ya kutoka (i) Ikoma mpaka Musoma kupitia Fort Ikoma, Nata, Ikizu na Musoma; (ii) Rungabure mpaka Seronera kupitia Nata na Ikoma, kama ilivyo leseni ya sasa. (163)

5810—Messrs. Martinus Atendo Odingo & Brothers, S.L.P. 124, Tarime. Ombi la leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 31 katika njia ya kutoka Nyamangaoro mpaka Musoma kupitia Sokorabolo na Utegi. (108)

5811—Musoma Bus Service Ltd., S.L.P. 50, Musoma. Ombi la kubadilisha Time-table kutoka Musoma saa 5.30 asubuhi badala ya saa 1.00 asubuhi na kutoka Ikoma saa 1.00 asubuhi badala ya saa 2.00 asubuhi. (65)

5812—Haji Sadiki Omari, S.L.P. 5, Geita. Ombi la leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 56 katika njia ya kutoka Butundwe/Bukondo mpaka Bukoli kupitia Kikobe, Kigunga, Nyakagomba, Nyansembe, Kibingo na Geita. (175)

5813—John Foya & Bros., S.L.P. 698, Mwanza. Ombi la leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 42 katika njia ya kutoka Kahangara mpaka Malampaka kupitia Magu, Kabila, Ndagalu, Nyambiti, Ngudu na Malya.

5814—John Foya & Bros., S.L.P. 698, Mwanza. Ombi la leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 62 katika njia ya kutoka Bunda mpaka Shinyanga kupitia Nassa, Ngasamo, Nguriati, Luguru, Maswa, Seke, Malampaka, Mondo na Kolandoto. (MZ/5813)

5815—John Foya & Bros., S.L.P. 698, Mwanza. Ombi la leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 42 katika njia ya kutoka Nyakabindi mpaka Nassa kupitia Ngasamo. (MZ/5813)

5816—Ismail Alli, S.L.P. 53, Sengerema. Ombi la kuendeleza leseni kwa gari moja la abiria 52 katika njia ya Msalala mpaka Geita kupitia Nyarubere, Nyanguhale, Chabaka na Buharara, kama ilivyo leseni iliyomalizika. (5)

5817—Bedri Said, S.L.P. 864, Mwanza. Ombi la kuongeza (i) gari moja la abiria 56 katika njia ya kutoka Mwanza/Shinyanga kupitia Misungwi, Ngudu, Malya, Maswa na Lalago (kila siku kutoka kila upande). Leseni ya sasa: angalia ombi Nambari MZ/5360. (166)

5818—Grewal Enterprise, S.L.P. 66, Musoma. Ombi la leseni ya mizigo kwa gari moja la tani 9 na gari moja la tani 7 katika barabara za (a) Musoma mpaka Arusha kupitia Mwanza na Singida; (b) Mkoa wa Mara.

5819—Lucas K. Nungu, S.L.P. 235, Musoma. Ombi la leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 62 katika njia ya kutoka Musoma mpaka Mugumu kupitia Busegwe na Nata.

MZ/5820—Jackson M. Mwita, S.L.P. 313, Musoma. Ombi la kuongeza njia ya kutoka Kiagata mpaka Musoma kupitia Makutano. Leseni ya sasa: angalia ombi Nambari MZ/5057. (186)

5821—Tarlochohan Singh, S.L.P. 66, Musoma. Ombi la leseni ya mizigo kwa gari moja la tani 7½ katika barabara za Mikoa ya Mwanza na Mara. (230)

5822—Ahmed Khalfan Al-jabry, S.L.P. 142, Shinyanga. Ombi la kuongeza (i) njia ya Igurubi mpaka Mwamashinga kupitia Igogo na (ii) kuondoka Shinyanga saa 7.30 mchana. Leseni ya sasa: angalia ombi Nambari MZ/5621. (294)

5823—Ismael Shaka Makonda, S.L.P. 82, Nzega. Ombi la leseni ya mizigo kwa gari moja la tani 7 katika barabara za Mikoa ya Tabora, Shinyanga na Mwanza.

5824—Fatma H. Ladha, S.L.P. 10, Nzega. Ombi la leseni ya mizigo kwa gari moja la tani 7 katika barabara za Mikoa ya Tabora, Shinyanga na Mwanza.

5825—Messrs. Uhuru Service Store, S.L.P. 10, Kahama. Ombi la leseni ya mizigo kwa gari moja la tani 7 katika barabara za Mikoa ya Shinyanga, Tabora na Kigoma. (88)

5826—Messrs. Vrajlali's, S.L.P. 205, Mwanza. Ombi la kuendeleza leseni ya mizigo kwa magari matano ya tani 7, gari moja la tani 5, magari mawili ya tani 11 na magari matano ya tani 10 katika barabara za Wilaya za Mwanza, Maswa na Geita, kama ilivyo leseni ya sasa. (212)

5827—Kahama Express Bus Services Ltd., S.L.P. 116, Kahama. Ombi la leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 52 katika njia ya kutoka Kahama mpaka Ushetu kupitia Ukune, Igusule na Isagehe.

BK/2141—Jamhuri Transport Bus Service Co., S.L.P. 208, Bukoba. Ombi la leseni ya abiria kwa magari mawili ya abiria 55 katika njia ya kutoka Bukoba mpaka Kabanga kupitia Kyaka, Bugene, Rulenge na Ngara Boma. (74)

2142—Jamhuri Transport Bus Service Co., S.L.P. 208, Bukoba. Ombi la kuendeleza leseni ya abiria kwa gari moja la abiria 50, magari mawili ya abiria 55 na gari moja la abiria 44 katika njia ya kutoka (a) Mtukula mpaka (i) Kabanga kupitia Kyaka, Bugene na Rulenge (mara nne kwa juma kutoka kila upande); (ii) Shanga kupitia Bukoba, Kanazi, Biharamulo, Lushahunga, Bulenge, Nyamwaga, Kabanga, Murukurazo na Ngara Boma (mara tatu kutoka kila upande) na (b) Murongo mpaka Bukoba kupitia Kaisho, Bugere na Kyaka; (iii) Nyaishozi mpaka Bukoba kupitia Bugene na Kyaka, kama ilivyo leseni ya sasa. (74)

2143—Selestin Rwabizi, S.L.P. 311, Bukoba. Ombi la kuongeza njia ya kutoka Nshamba mpaka Birabo. Leseni ya sasa: angalia ombi Nambari BK/1824. (144)

2144—African Bus Service, S.L.P. 932, Mwanza. Ombi la kuongeza (i) gari moja la abiria 66 na (ii) njia Mabamba mpaka Karumo kupitia Kibondo, Lushahunga, Biharamulo, Lunazi na Geita. (67)

2145—African Bus Service, S.L.P. 932, Mwanza. Ombi la kuongeza (i) gari moja la abiria 66 na njia (ii) Bukoba mpaka Murusumo kupitia Kyaka na Karagwe. (67)

2146—Mohamed Mtoro Kabeya, S.L.P. 349, Bukoba. Ombi la kuongeza gari moja la abiria 51 na njia ya kutoka Ruzinga mpaka Bukoba kupitia Buyango, Kashasha, Bugandika, Rukurungo, Gera na Kagege. Leseni ya sasa: angalia ombi Nambari BK/1923. (14)

MAOMBI YA LESENI ZA MUDA

84/72—Mohamed Mzee, S.L.P. 9124, Dar es Salaam. Ombi la leseni ya muda kwa gari moja la abiria 52 katika njia ya kutoka Dar es Salaam mpaka Kitondwe kupitia Kisarawe, Masaki, Kibuta na Chang'ombe. (DS/6039)

85/72—Mzee Mbwana Seseme, S.L.P. 15098, Dar es Salaam. Ombi la leseni ya muda kwa gari moja la abiria 45 katika njia Chasimba mpaka Dar es Salaam kupitia Mkoga, Sanganzeru na Samvula Chole. (267)

E. R. M. BALELE,
k.n.y. Katibu,
Baraza la leseni za Usafirishaji

Dar es Salaam,
7 Oktoba, 1972

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 1480 2/D/3

BARAZA LA LESENI ZA USAFIRISHAJI

KUSIKILIZA MAOMBI

Watu wote wanajulishwa ya kwamba kutokana na Kifungu cha 8 cha Sheria za Umilikaji Leseni, Baraza la Leseni za Usafirishaji litafanya mikutano ya hadhara kusikiliza maombi ya watu wanaoomba leseni za barabara, kupakia mizigo na kubadilisha leseni katika mahali na tarehe kama ifuatavyo hapa chini.

Watu wote wanaohusika na maombi haya au kupinga wanashauriwa kuhudhuria.

Tabora: (Parish Hall). Maombi ya Mkoa wa Tabora yatasikilizwa siku zifuatazo:—

Jumatatu tarehe 23 Oktoba na Jumanne tarehe 24 Oktoba, 1972. Mkutano huanza saa 8 mchana Jumatatu na saa 2.30 asubuhi Jumanne.

Kigoma: (District Council Chamber). Maombi ya Mkoa wa Kigoma yatasikilizwa siku zifuatazo:—

Jumatano tarehe 25 Oktoba, 1972 saa mbili na nusu asubuhi.

Bukoba: (Red Cross). Maombi ya Mkoa wa Ziwa Magharibi yatasikilizwa siku zifuatazo:—

Alhamisi tarehe 26 Oktoba, saa mbili na nusu asubuhi. Ijumaa tarehe 27 Oktoba, saa mbili na nusu asubuhi.

Mwanza: (Jumba la Gandhi). Maombi ya Mkoa wa Mwanza yatasikilizwa siku zifuatazo:—

Jumamosi tarehe 28 Oktoba, saa mbili na nusu asubuhi.
Jumapili tarehe 29 Oktoba, saa mbili na nusu asubuhi.
Jumatatu tarehe 30 Oktoba, saa mbili na nusu asubuhi.

UTARATIBU

Maombi yote yaliotangazwa katika *Gazeti* la Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 16 Juni, 23 Juni, 21 Julai, 28 Julai, 11 Agosti, 25 Agosti, 15 Septemba, 22 Septemba na kwenye magazeti mengine kabla ya mkutano.

Transport Licensing Authority,
P.O. Box 1910,
Dar es Salaam.
30 Septemba, 1972

H. A. KILUVIA.
Katibu,
Baraa la Leseni za Usafirishaji

TAARIFA YA KAWAIDA Na. 1481

MAKAMPUNI YANAYOTARAJIWA KUFUTWA KATIKA DAFTARI LA MAKAMPUNI

Sheria ya Makampuni

(Sura ya 212)

Inatolewa ilani chini ya kifungu 283 (3) cha Sheria ya Makampuni kwamba baada ya miezi mitatu kutoka tarehe ya ilani hii majina ya makampuni yafuatayo yatafutwa katika Daftari la Makampuni iwapo hakutakuwa na kipingamizi cho chote kabla ya miezi hiyo mitatu kupita.

PLASTRADE TANZANIA LIMITED.
HIGHWAYS PROPERTIES LIMITED.
AMANA MINING CORPORATION LIMITED.
ATLAS CONTRUCTION LIMITED.
AL-BARKAT HOUSE LIMITED.
MVUMI SISAL ESTATE LIMITED.
DESBRO (TANZANIA) LIMITED.
LAKE COFFEE ROASTERS AND PACKERS LIMITED.
WAZO FARM LIMITED.
MONE TARY AGENCIES (TANZANIA) LIMITED.
MODE PROPERTIES LIMITED.
HAPPY FLATS LIMITED.
AFRO MARKETING SERVICES (TANGANYIKA) LIMITED.
TANZANIA DECORATORS LIMITED.
ACROPOL HOTEL LIMITED.
MWANANCHI HOLDINGS LIMITED.
WATINGINYA TRADING COMPANY LIMITED.
UNITED MINING COMPANY LIMITED.
MAKIBA ESTATES LIMITED.
ABDUL MOHAMED & BROS. LIMITED.
KENTA MINES LIMITED.

Dar es Salaam,
5 Oktoba, 1972

K. KOBELO,
Msajili Msaidizi wa Makampuni

TAARIFA YA KAWAIDA Na. 1482

MTUMIZI WA ALAMA YA BIASHARA

Sheria ya Alama ya Biashara

(Sura ya 394)

Tangazo linatolewa kwamba Mtumizi wa Alama ya Biashara ameandikishwa katika Daftari ya Uandikishaji wa Alama za Biashara kama ifuatavyo:—

Jina la mwenye mali: Fleer Corp.
Anwani: 10 Street and Somerville Avenue, City of Philadelphia, State of Pennsylvania 19120, United States of America.
Jina la mtumiaji: Fleer G.m.b.H.
Anwani: 54 Industrie Strasse 6909 Waldorf/Baden, Germany.
Anwani ya utumishi: Dharsee & McRoberts, Wawakilishaji, S.L.P. 2091, Dar es Salaam.
Nambari ya alama ya biashara na bidhaa zake: 6607 kwa ajili ya bidhaa kama ilivyoonyeshwa katika uandikishaji.
Masharti: Kama ilivyo katika mapatano yaliyotiwa sahihi baina ya mwenye mali na mtumizi tarehe 2 Februari, 1971.

Dar es Salaam,
29 Septemba, 1972

K. KOBELO,
Msaidizi Msajili wa Alama za Biashara

TAARIFA YA KAWAIDA Na. 1483

TANGAZO LA KUUZA BIASHARA

Sisi Tanganyika Umoja Trading Company Limited, tunatoa tangazo kwamba biashara iliyokuwa ikiendeshwa na sisi hapa Moshi, tumeuza na kubadilisha kwa SADRUDIN NANJI JIWA wa hapa Moshi, ambaye ataendelea na biashara hiyo. Sisi tutakuwa na madaraka kuhusiana na biashara hiyo kuishia tarehe 20 Septemba, 1972. Tutahusika na madeni (ikiwa yapo) ya biashara hiyo mpaka tarehe 20 Septemba, 1972.

Zaffer Ali,
Advocate,
P.O. Box 246,
Moshi

A. M. LASWAI,
Director
Mwenye Biashara

TAARIFA YA KAWAIDA Na. 1484

TAARIFA

Hii ni taarifa ya kuwajulisha Customers wetu wajulikanao ambao wameacha radio, tape recorders, gramophones, vitu vya umeme na vitu vingine vya kufanyia ripea pamoja na sisi, mje mchukue vitu vyenu pamoja na malipo yetu kabla ya tarehe 30 Oktoba, 1972. Vitu visipochukuliwa kwa muda huu utajwao vitauzwa kwa ajili ya gharama ya utengenezaji na malipo na uwekaji na gharama zinginezo.

S.L.P. 341,
Bukoba,
16 Septemba, 1972

U. H. MEHTA,
Mwenye Kuhusika

KWENDA LIKIZONI

Jina	Cheo	Stesheni	Sababu ya Kuondoka	Tarehe
B. M. JUMA	Mwenyekiti, Tume ya Utumishi wa Vyama vya Ushirika, Ujima	Dar es Salaam	Likizo	11 Sept., 1972
L. MFALILA	Kaimu Jaji, Mahakama Kuu	Dar es Salaam	Likizo	1 Okt., 1972

UHAMISHO

Jina	Cheo	Kutoka	Kwenda	Tarehe
F. MSUKU	Ofisa Mwangalizi, Wizara ya Uchumi	Uchumi, Dar es Salaam	Waziri Mkuu, Dar es Salaam	7 Sept., 1972

KUACHA KAZI

Jina	Cheo	Stesheni	Sababu	Tarehe
A. K. MWASORA	Bwana Afya Mkuu wa Mifugo, Wizara ya Kilimo	Monduli	Kupumzika Kazi	5 Okt., 1972
D. S. MPANGIRI	Bwana Afya wa Mifugo, Daraja la I, Wizara ya Kilimo	Dodoma	Kuacha Kazi kwa ajili ya Ugonjwa	1 Okt., 1972
J. KUHAMWA	Bwana Afya Msaidizi wa Mifugo, Daraja la II, Wizara ya Kilimo	Maswa	Kupumzika Kazi	1 Okt., 1972
J. FIEDLER	Afisa Mganga wa Mifugo, Daraja la II, Wizara ya Kilimo	Tabora	Kumalizika kwa Mkataba	2 Okt., 1972
V. GONDWE	Mkaguzi Mdogo wa Polisi, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi	Tanga	Kujiuzulu Kazi	6 Okt., 1972
J. S. M. KISHALULI	Executive Officer, Wizara ya Mali ya Asili na Utalii	Dar es Salaam	Kuacha Kazi	1 Okt., 1972

MASAHIHISHO

Vol. LIII, *Gazeti* Na. 13 la tarehe 31 Machi, 1972—Taarifa ya Kawaida Na. 500—Jina la Mtahiniwa Na. Q.16 *Lisomeke* "Bi. M. S. MUSHALA".

Vol. LIII, *Gazeti* Na. 27 la tarehe 7 Julai, 1972—Taarita ya Kawaida Na. 946—Chini ya Kuajiriwa na Kukabidhiwa Madaraka—Neno "Tume" *lisomeke* "Tume ya Utumishi Serikali za Mitaa—na cheo cha C. R. MLOKA, *kisomeke* "Executive Officer".

Vol. LIII, *Gazeti* Na. 38 la tarehe 22 Septemba, 1972—Taarifa ya Kawaida Na. 1340—Chini ya Kuajiriwa na Kukabidhiwa Madaraka. Wizara ya Biashara na Viwanda—A. J. ZIDIKHERI, tarehe ya kuanzia cheo hicho *isomeke* "27 Desemba, 1968".

Vol. LIII, *Gazeti* Na. 39 la tarehe 29 Septemba, 1972—Taarifa ya Kawaida Na. 1387—Chini ya Kuajiriwa na Kukabidhiwa Madaraka—Idara ya Mahakama—S. N. BIDEBERI amepandishwa cheo kuwa "Hakimu wa Wilaya, Daraja la II".

Vol. LIII, *Gazeti* Na. 39 la tarehe 29 Septemba, 1972—Taarifa ya Kawaida Na. 1387—Chini ya Kuajiriwa na Kukabidhiwa Madaraka—Idara ya Mahakama—"Bwana A. I. BALOZI" amepandishwa cheo kuwa "Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo, Daraja la I".

Vol. LIII, *Gazeti* Na. 39 la tarehe 29 Septemba, 1972—Chini ya Waliothibitishwa Kazini—Wizara ya Kilimo—(a) "Bwana Shamba Msaidizi Daraja la III", *lisomeke* "Mr. M. JUMA, Bwana Afya Msaidizi wa Mifugo". (b) "O. KOMBA"; *lisomeke* "Q. KOMBA".

Vol. LIII, *Gazeti* Na. 39 la tarehe 29 Septemba, 1972—Taarifa ya Kawaida Na. 1387—Chini ya Kuajiriwa na Kukabidhiwa Madaraka—Majina yafuatayo *yasomeke* chini ya "Wizara ya Mali ya Asili na Utalii":—

P. Y. NYITI, Afisa wa Nje, Daraja la II.

J. D. KYANDO
D. MNALIMI
L. M. DOGANI
E. P. SHAYO
E. S. AKYOO
S. M. S. NAMIMUYA
} Mabwana Miti Wasaidizi, Daraja la II.

Hupigwa Chapa na Mpigachapa Mkuu wa Serikali, Dar es Salaam, Tanzania.